# UCHANGANUZI LINGANISHI WA SWALA LA MAADILI KWA VIJANA WA KIUME KATIKA TENZI MBILI: *SIRAJI* NA *ADILI*

**NA**

**GWAKO BOSIBORI JACKLINE**

**C50/72355/2014**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya aina yoyote katika chuo kikuu chochote kingine.

Sahihi……………………………………………Tarehe ………………………………

**Gwako Jackline**

**(Mtahiniwa)**

**Nambari ya Usajili: C50/72355/2014**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi……………………………………………Tarehe ………………………………

**Prof. Rayya Timammy**

Sahihi……………………………………………Tarehe ………………………………

**Dr. Hezron Mogambi**

## TABARUKU

Kwa mamangu mpendwa Janes Kerubo na marehemu babangu Benson Gwako kwa kunilea na kunipigania nipate elimu. Pia kwa mume wangu Abel Nyarang'o ambaye alinitia moyo hadi mwisho pamoja na mtoto wangu Meyer Kerubo.

**SHUKURANI**

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mola kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu. Aidha shukrani za dhati ni kwa wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Dkt. Hezron Mogambi kwa uelekezi mwafaka walionipatia katika harakati za uandishi wa tasnifu hii. Mola awazidishie hekima na maarifa zaidi.

Mbali na hao, ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wa Idara ya Kiswahili kwa msingi thabiti walionipa na maarifa yao chungu nzima yaliyochangia kufanikisha utafiti wangu. Hawa ni pamoja na: Prof. Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof Mwenda Mbatia, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt Amiri Swaleh na Dkt Mbuthia. Mungu awabariki.

Sitawasahau wanafunzi wenzangu tuliosoma nao na kusaidiana kwa njia moja au nyingine; na kutiana moyo wakati mambo yanaonekana kuwa magumu. Hawa ni pamoja na Virginia Wairimu, Sarah Kivuva, Seraphine Kemuma, Winnie Awour, Dorcas Suita, Tecla Kiptum, James Kimwea, Godfrey Makori, Jonh Mugo, miongoni mwa wengine.

Kwa ndugu zangu Laban, Tabitha, Dorice, Japhet, Druscillah, Reuben, Fridah na Askah kwa kunistahamilia na pia kwa malezi ya mwanangu nilipokuwa masomoni. Sitamsahau Ustadhi Mahmoud Abdulkadir (MAU) kwa mchango wake wa vitabu na mawaidha yake yaliyochangia kufanikisha kazi hii. Vilevile walimu wenzangu nawashukuru kwa kunipa wakati mwafaka kazini kutokana na usaidizi wa kila aina.

Hatimaye ninamshukuru mama yangu Janes Kerubo pamoja na marehemu baba yangu Benson Gwako kwa maadili walionipa na kunitia moyo kila wakati ili kufanya bidii masomoni pamoja na mume wangu Abel Nyarango na mwanangu Meyer Kerubo aliyepata wakati mgumu kunikosa kila mara nikiwa masomoni. Shukrani kwa baba mkwe Omariba na mama mkwe Alice. Pengine sikuweza kuwataja wote walionifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote ahsante kwa kunifaa na Mungu awabariki.

## IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia maadili kwa vijana wa kiume yanayojitokeza katika tenzi za *Siraji* na *Adili*. Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya maadili ambayo inalenga kazi za fasihi kutatua matatizo ya jamii kwa njia ipasavyo na kujenga jamii bora yenye maelewano. Malengo ya utafiti wetu ni kuangalia jinsi ambavyo watunzi Kijumwa na Robert wa utenzi *Siraji* na *Adili* wamelishughulikia swala la maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi hizo. Aidha, tumelinganisha na kulinganua jinsi watunzi Kijumwa na Robert wamelishughulikia swala la maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi hizo na hatimaye tumebaini sababu za kuwiana na kutofautiana kwao. Baada ya kufanya utafiti wetu kwa kusoma na kuzichambua tenzi- *Siraji* na *Adili* tumebaini ya kwamba makisio yetu kuwa watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia maadili kwa vijana wa kiume ni ukweli na pia wamewiana na kutofautiana kwa njia moja au nyingine. Hatimaye tumeweza kubaini ya kwamba ni ukweli tenzi hizi zina uhusiano wa karibu sana kwa sababu watunzi Kijumwa na Robert wameyafungamanisha maadili hayo na mafunzo ya dini ya Kiislamu ndiposa tukachanganua data yetu kwa njia ya maelezo na ufafanuzi huku tukitoa thibitisho kutoka kwa tenzi- *Siraji* na *Adili* pamoja na *Kurani Takatifu*. Aidha, tumepata kuwa kutofautiana kwa watunzi kunatokana na maoni yao ya kibinafsi, na tajriba walionazo kutegemea mazingira waliokulia.

## YALIYOMO

UNGAMO.......................................................................................................... ii
TABARUKU.......................................................................................................... iii
SHUKURANI.......................................................................................................... iv
IKISIRI ..........................................................................................................v
YALIYOMO .......................................................................................................... vi
VIFUPISHO..........................................................................................................x

**SURA YA KWANZA..........................................................................................................1**
1.0 Utangulizi..........................................................................................................1
1.1 Tatizo la utafiti ..........................................................................................................2
1.2 Maswali ya utafiti ..........................................................................................................3
1.3 Madhumuni ya utafiti..........................................................................................................3
1.5 Upeo na mipaka ..........................................................................................................5
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti ..........................................................................................................5
1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti katika ushairi .......................................... 6
1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada katika kazi zingine ................................................ 7
1.7 Msingi wa kinadharia wa utafiti ..........................................................................................................9
1.7.1 Nadharia ya maadili .......................................................................................... 9
1.8 Mbinu za utafiti..........................................................................................................14
1.8.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli .......................................................................... 14
1.8.2 Ukusanyaji data na mbinu za ukusanyaji data .................................................... 14
1.8.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ................................................................ 14
1.9 Muhtasari ..........................................................................................................15

**SURA YA PILI..........................................................................................................16**
**DHANA YA MAADILI NA YANAYOJITOKEZA.......................................................16**
**KATIKA UTENZI WA *SIRAJI* NA *ADILI* ..........................................................16**
2.0 Utangulizi..........................................................................................................16
2.1 Dhana ya kijana..........................................................................................................16

2.2 Dhana ya maadili ....................................................................................17
2.3 Dhima ya maadili....................................................................................19
2.4 Maadili yanayojitokeza katika utenzi wa *Siraji.*..............................................21
2.4.1 Dini na imani kwa Mungu .................................................................... 22
2.4.2 Adabu, utii na heshima......................................................................... 23
2.4.3 Elimu..................................................................................................... 25
2.4.4 Wema na utu......................................................................................... 26
2.4.5 Tamaa ................................................................................................... 26
2.4.6 Ukarimu ............................................................................................... 27
2.4.7 Mapenzi ya dhati................................................................................... 28
2.4.8 Kuwa na subira .................................................................................... 29
2.4.9 Kuwa na ulimi mzuri ............................................................................ 30
2.4.10 Bidii kazini.......................................................................................... 30
2.4.11 Ndoa ................................................................................................... 31
2.5 Maadili yanayojitokeza katika utenzi wa Adili...............................................33
2.5.1 Dini na imani kwa Mungu .................................................................... 34
2.5.2 Heshima kwa wazazi na walimu............................................................ 36
2.5.3 Adabu na utii......................................................................................... 37
2.5.4 Umuhimu wa elimu............................................................................... 38
2.5.5 Bidii kwa kazi ....................................................................................... 39
2.5.6 Nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii.............................. 40
2.5.7 Ndoa na mapenzi ya dhati kwa watu ..................................................... 41
2.5.8 Utu wema na matendo mazuri .............................................................. 42
2.5.9 Kuwa na ulimi mzuri ............................................................................ 43
2.6 Hitimisho....................................................................................................44

**SURA YA TATU ..........................................................................................45**
**JINSI WATUNZI WA TENZI *SIRAJI NA ADILI* WANAVYOWIANA NA SABABU ZA KUWIANA KWAO..........................................................45**
3.0 Utangulizi....................................................................................................45
3.1 Maadili yanayowiana katika tenzi *Siraji* na *Adili* ...........................................45
3.1.1 Dini na imani kwa Mungu .................................................................... 45

3. 1.2 Elimu........................................................................................................ 48
3.1.3 Ndoa na mapenzi................................................................................................ 49
3.1.4 Bidii kazini........................................................................................................ 50
3.1.5 Uwajibikaji........................................................................................................ 51
3.1.6 Umakinifu ........................................................................................................ 53
3.1.7 Heshima na adabu ............................................................................................ 56
3.1.8 Utu wema na matendo mazuri ......................................................................... 58
3.1.9 Kuweka siri ....................................................................................................... 59
3.1.10 Malezi bora ...................................................................................................... 60
3.1.11 Ushirikiano na uhusiano mwema ..................................................................... 62
3.1.12 Msamaha ......................................................................................................... 63
3.1.13 Kuwa na upole ................................................................................................. 64
3.1.14 Uvumilivu ........................................................................................................ 66
3.2 Sababu za kuwiana kwa watunzi Kijumwa na Robert kwa jinsi wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume ..................................................................................... 67
3.3 Hitimisho.................................................................................................................68

**SURA YA NNE ..........................................................................................................69**
**JINSI WATUNZI WA TENZI *SIRAJI* NA *ADILI* WANAVYOTOFAUTIANA NA SABABU ZA KUTOFAUTIANA KWAO .....................................................................69**
4.0 Utangulizi.................................................................................................................69
4.1 Maadili katika utenzi wa *Siraji* yanayotofautina na ya utenzi wa *Adili* ......................69
4.1.1 Subira ................................................................................................................ 70
4. 1.2 Tabia za maakuli ............................................................................................... 71
4.1.3 Udaku na kusengenya ......................................................................................... 75
4.1.4 Haki na upatanisho.............................................................................................. 76
4.1.5 Ushahidi ............................................................................................................. 77
4.1.6 Kufariji................................................................................................................ 77
4.1.7 Tamaa ya vitu vya watu ....................................................................................... 78
4.1.8 Talaka ................................................................................................................. 79
4.1.9 Kutojishughulisha na mambo ya watu. ................................................................. 80
4.1.10 Utumizi kwa wenzake/ usaidizi .......................................................................... 80
4.2 Maadili katika utenzi wa *Adili* yanayotofautiana na ya utenzi wa *Siraji*.....................81

4.2.1 Ubinafsi ........................................................................................................ 81
4.2.2 Kutimiza ahadi ................................................................................................ 82
4.2.3 Chuki ............................................................................................................. 82
4.3 Sababu za kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert ........................................83
4.4 Hitimisho..........................................................................................................84

**SURA YA TANO......................................................................................................85**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..............................................................................85**
5.0 Utangulizi...........................................................................................................85
5.1. Muhtasari ..........................................................................................................85
5.2 Matokeo .............................................................................................................85
5.3 Mapendekezo ya utafiti zaidi ...............................................................................86
**MAREJEREO ...........................................................................................................87**

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| K. L.B | Kenya Literature Bureau |
| K.m. | Kwa mfano |
| Kijumwa | Mohammad Kijumwa |
| Robert | Shaaban Robert |
| Uk. | Ukurasa |
| Ub. | Ubeti |

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Fasihi ni taaluma inayohusu tungo za kisanaa za simulizi na andishi. Fasihi imegawika katika matawi mawili makuu ambayo yana tanzu zake. Kuna fasihi andishi k.m riwaya, tamthilia, tawasifu, wasifu, mashairi na nyinginezo. Aidha, kuna fasihi simulizi k.m hadithi, ngano na vitendawili zinavyosimuliwa kwa mdomo. Fasihi simulizi ndio chanzo cha fasihi andishi kwani ilikuja mwanzo kabla ya fasihi andishi.

Katika utafiti wetu tumejikita kwenye fasihi andishi katika utanzu wa ushairi. Ushairi una majukumu muhimu katika jamii na majukumu hayo ni pamoja na kuonya, kutahadharisha, kuelimisha, kuadilisha, kuwapevusha na kuwahamasisha wanajamii kuchukua mkondo wa mwelekeo wa vitushi ambao unaleta undugu na utangamano katika jamii. Kwa kufanya hivyo, basi fasihi huchangia kujenga uhusiano mwema kati ya wanajamii na kuleta mabadiliko katika maisha yao. Hata hivyo ushairi umepitia mabadiliko mengi sana ambayo hudhihirika kwa njia ya kimaudhui na kifani. Kufikia sasa kuna mashairi huru ambayo hayazingatii vina wala mizani kama yale ya awali. Tumeshughulikia moja katika bahari za ushairi ambayo ni utenzi. Utenzi ni miongoni mwa bahari za ushairi ambayo ni kongwe sana na una sifa ya urefu miongoni mwa sifa nyingine; aidha hutumiwa kusimulia visa au maudhui marefu yanayomkumba binadamu na maisha yake ulimwenguni.

Imebainika ya kuwa kazi nyingi za kifasihi zimeegemezwa kwenye misingi ya kimaadili ambapo zinafichua na kuchimbua maovu yaliyopo katika jamii kwa lengo la kujenga jamii bora. Katika utafiti wetu tumejikita katika maadili kwa vijana wa kiume katika utenzi wa *Siraji* na *Adili* ili kubaini ni kwa jinsi gani ambavyo watunzi Kijumwa na Robert wamefanikiwa kuonya, kuelimisha na kutahadharisha jamii dhidi ya maovu.

Utenzi wa *Siraji* ulitungwa mwaka wa 1927 na mtunzi Mohammad Kijumwa. Utenzi huu una beti 209 na unahusu wasia wa Kijumwa kwa mwanaye ambao umefungamanisha mafunzo ya dini na mawaidha ya kijamii. Aliutunga kwa mwanaye wa kiume Helewa ili kuyatumia katika maisha na kuyaeneza kwa wanajamii wengine. Kijumwa amempa kijana wake Helewa

mawaidha ya jinsi ya kuishi katika jamii ili kujenga uhusiano mwema na Mungu na pia na wanajamii kwani bila Mungu hakuna aliwezalo mwanadamu katika maisha yake. Amemshauri kushika mawaidha hayo na kuyatumia katika harakati zake za kila siku kuanzia akiwa kijana mdogo, atakapooa na pia akiwa mzazi. Aidha, amemshauri jinsi ya kujenga uhusiano mwema kati yake na watu wa ukoo, majirani, marafiki, maskini na matajiri bila kusahau watu walemavu.

Utenzi wa *Adili* ulitungwa na mtunzi maarufu Shaaban Robert na kuhifadhiwa kwenye diwani ya *Pambo la Lugha* (1966). Utenzi huu una beti 100. Katika utenzi huu anamwusia kijana wake wa kiume Adili. Mwandishi Shaaban Robert amemwelekeza kijana wake kuwa na maadili ya kumwongoza katika maisha yake. Amemshauri kumcha Mungu, kuwa na adabu na utii, kuwa na heshima kwa wazazi, kuepuka uvivu, fitina, umuhimu wa elimu, kujitunza, kuchunga wakati, uvumilivu na mapenzi ya dhati katika ndoa na mengineyo mengi. Maswala ambayo yameshughulikiwa na watunzi hawa wawili yana majukumu muhimu ya kuwatahadharisha na kuwaelekeza vijana katika harakati zao za maisha.

Tulizichagua tenzi- *Siraji* na *Adili* kwa sababu zina uhusiano wa karibu sana na hazijarejelewa sana na wahakiki waliotangulia. Mawaidha ambayo watunzi Kijumwa na Robert wametoa kwa wana wao yamefungamanishwa na mafunzo ya dini ya Kiislamu na lengo lao kuu ni kwamba mawaidha hayo yatawaelekeza kuishi vyema na kuwa vielelezo vyema kwa wanajamii wenzao hivyo basi kuadilisha jamii. Ni dhahiri kwamba watunzi hao wawili waliyaangazia matatizo katika jamii zao mahususi ndipo wakaonelea kutafuta suluhisho ya matatizo hayo.

## 1.1 Tatizo la utafiti

Kwa vile maadili ni kigezo muhimu katika kufaulu maishani, ni sharti kila mzazi awajibike katika kutilia mkazo maadili kwa mwanaye kuanzia utotoni hadi pale anapokuwa mtu mzima. Vijana wanachukua sehemu muhimu sana katika jamii kwani ndio msingi na tegemeo la taifa katika siku zijazo. Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyonukuliwa katika gazeti la Taifa Leo tarehe 17.10.2015 inasema kwamba idadi kubwa ya vijana hasa wa vyuo vikuu wanajiunga na ugaidi kwa kuahidiwa kitita cha pesa. Aidha katika nchi yetu ya Kenya, vijana wamekumbwa na changamoto nyingi kama zile za kutumia mihadarati, uvutaji sigara, ulevi na ukosefu wa ajira

miongoni mwa nyinginezo. Hili ni thibitisho tosha kuwa kuna upungufu wa madili miongoni mwa vijana.

Hivyo, tatizo la utafiti wetu ni kuchunguza na kubainisha jinsi maadili ya vijana wa kiume yanajitokeza katika tenzi mbili- *Siraji* na *Adili*. Tumechunguza mchango wa watunzi Kijumwa na Robert katika kuwaelekeza na kuwatahadharisha vijana wa kiume na wajibu wa maadili hayo. Utafiti huu umelenga kulinganisha na kulinganua jinsi watunzi Mohammad Kijumwa na Shabaan Robert wameshughulikia maadili ya vijana wa kiume na hatimaye kuchunguza sababu za kuwiana na kutofautiana kwao. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya kimaadili ambayo inasisitiza fasihi kuwa na wajibu wa kuadilisha jamii; aidha nadharia hii inahusu kiini kilichomo katika utendaji ulio sawa na usio sawa.

### 1.2 Maswali ya utafiti

Utafiti wetu umeongozwa na maswali yafuatayo:

a) Je, watunzi Kijumwa na Robert wa utenzi wa *Siraji* na *Adili* wameyashughulikia maadili kwa vijana wa kiume?
b) Je, watunzi hawa wanawiana na kutofautiana kwa jinsi ambavyo wameshughulikia suala la maadili kwa vijana wa kiume?
c) Je, kufanana na kutofautiana kwa watunzi hawa kumetokana na sababu zipi?

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

Lengo kuu la utafiti wetu ni kuchunguza jinsi ambavyo watunzi Kijumwa na Robert wameshughulikia swala la maadili kwa vijana. Basi, tunalenga kutathmini namna waandishi hawa wamewiana na kutofautiana katika kazi zao. Malengo ya utafiti wetu hasa ni:

a) Kuangalia namna Mohammad Kijumwa na Shaaban Robert wamelishughulikia swala la maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi zao.
b) Kulinganisha na kulinganua jinsi watunzi hao wawili wamelishughulikia swala la maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi zao.
c) Kubaini sababu za kuwiana na kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert.

**1.4 Sababu za kuchagua mada hii.**

Kuna upungufu wa maadili miongoni mwa vijana katika jamii ya sasa. Mambo ambayo yanashuhudiwa miongoni mwao ni: ulevi, uvutaji sigara, matumizi ya mihadarati, migomo kwenye vyuo vikuu vya masomo na shule za sekondari, kujiunga na ugaidi na uhalifu wa kila aina. Ingawa vijana hawa wanawakilisha asilimia kubwa nchini Kenya na ndio tegemeo la uhai wa taifa katika siku zijazo, wanakumbwa na changamoto nyingi sana. Hivyo tulivutiwa na tenzi hizi *Siraji* na *Adili* ili kuchunguza jinsi ambavyo watunzi Kijumwa na Robert waliyashughulikia maadili ya vijana wa kiume katika tenzi zao.

Kulingana na ufahamu wetu, tenzi hizi hazijarejelewa kwa wingi sana na wasomaji na hatukuweza kupata mhakiki aliyeshughulikia maadili ya vijana wa kiume katika tenzi hizi za *Siraji* na *Adili.* Tenzi ni za zamani na kutokana na sifa zao za urefu na lugha iliyotumika, huenda zikadharauliwa hasa na vijana kwamba zimepitwa na wakati. Pia kwa vile kuna mashairi ya kisasa yanayowavutia zaidi hivyo vijana kukosa ujumbe muhimu unaofaa kuwapa mwelekeo mwema na kuwaongoza maishani. Hivyo, katika utafiti wetu tunanuia kuwadondolea wasomaji maadili hayo na kuyaweka wazi kwa wasomi ili kuyasisitiza yale yanayowafaa katika jamii kuyafuata ili kuepukana na kuzorota kwa maadili katika jamii.

Kuchangia katika taaluma ya kiusomi kwa kuendeleza fasihi andishi. Kutokana na ufafanuzi wetu tunatumai kwamba wasomi watachangamkia zaidi kusoma tenzi hizi na nyingine kisha baadaye kuzitafiti sehemu ambazo bado hazijashughulikiwa ili kukuza lugha ya Kiswahili na kuendeleza fasihi andishi.

Wamitila (2003:55) anasema kuwa matukio hayatokei tu bali hutokea kwa kuwa mwandishi anataka kuliendeleza swala fulani au ana nia fulani maalumu. Tunakubaliana na mtaalamu huyu ndiposa tukachagua tenzi hizi *Siraji* na *Adili* kuhakiki swala la maadili ambapo tunapata kwamba lengo la watunzi Kijumwa na Robert ni kuwaelekeza vijana wao wa kiume kuwa na utu. Hivyo tumebainisha shabaha za tungo hizo. Kazi hii inanuia kuongeza maarifa katika uwanja wa tendi za kiafrika. Tunatumai kwamba kazi yetu itazidi kupanua mawanda ya tendi baada ya kuandika

kile kilichoachwa na wasomi wengine katika uwanja huu na kupendekeza utafiti kufanywa zaidi katika sehemu ambazo hazijatafitiwa.

## 1.5 Upeo na mipaka

Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza na kubainisha mchango wa watunzi Kijumwa na Robert katika kuwaelekeza vijana wao wa kiume kuyatambua mazuri na mabaya maishani kupitia tenzi zao. Utenzi wa *Siraji* wa mtunzi Mohamed Kijumwa una beti 209 na utenzi wa *Adili* wa mtunzi Shaaban Robert una beti 100. Tenzi hizi mbili zilitungwa kama wasia kwa vijana wa kiume ambao ni Helewa na Adili. Tumepitia tenzi hizo kwa lengo la kutambua maadili waliyoyashughulikia kuwaongoza vijana wa kiume kwa jumla na kuyalinganisha na kuyalinganua. Pia tumepata ya kwamba mtunzi Kijumwa katika utenzi *Siraji* ameyashughulikia maadili kwa vijana wa kike katika beti chache sana hivyo nasi hatuna budi kuyagusia japo si kwa undani. Aidha tumechunguza sababu za kuwiana na kutofautiana kwao ingawa hatujashughulikia swala la fani au mtindo katika utafiti wetu.

Tumejikita katika nadharia ya maadili ambayo inasisitiza fasihi kuwa na wajibu wa kuadilisha jamii na pia inalenga kubainisha kilichomo ndani ya vitendo kuvifanya viwe sawa au visiwe sawa. Nadharia ya maadili inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kujenga jamii bora yenye maelewano kwa kuangalia kazi za kifasihi na ubinadamu na hasa maswala ya kimaadili. Hivyo kwa kutilia maanani mawazo hayo tumevitumia vipengele vya nadharia ya maadili kubainisha na kuchanganua mchango wa watunzi wa utenzi wa Kijumwa *Siraji* na ule wa Robert *Adili* tukizingatia maadili miongoni mwa vijana na umuhimu wa maadili hayo katika jamii.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti

Katika sehemu hii tumesshughulikia kazi ambazo zina uhusiano na mada yetu ya utafiti pamoja na nadharia ya maadili iliyotuelekeza katika utafiti wetu. Ingawa hatukuweza kuona kazi ambazo zinashughulikia suala la maadili ya vijana wa kiume kwa kulinganisha tenzi hizi mbili za *Siraji* na *Adili*, tumepitia kazi tofautitofauti ambazo zinashughulikia masuala ya vijana kwa kujikita katika ushairi na zingine katika riwaya na tamthilia pia.

Mbali na utafiti wetu kuna tafiti nyingi zimefanywa kwa kushughulikia maswala ya vijana isipokuwa kwa njia tofauti na kwa kujikita kwenye nadharia tofauti; aidha uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba wapo wataalamu walioshughulikia utenzi wa *Siraji* na ule wa *Adili* ila kile walichokishughulikia ni tofauti na chetu. Sehemu hii tumeigawa katika vijimada viwili vifutavyo: Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti katika ushairi na yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti katika kazi zingine.

### 1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti katika ushairi

Abou Egl, (1983) ameshughulikia maisha ya mtunzi Kijumwa na kazi zake. Katika tasnifu yake ya uzamifu aliyoifanya katika chuo kikuu cha London ameshughulikia maisha ya Kijumwa na utunzi wake na pia kazi zake zingine za usanii. Aidha ameshughulikia nyimbo na tenzi za Kijumwa, utenzi wa *Siraji* ukiwemo. Kazi yake imetufaa sana kwa kutupa mwongozo kumwelewa zaidi mtunzi Kijumwa na falsafa ya maisha yake. Aidha tumepata kuelewa utenzi wa *siraji* ambao tumeushughulikia pamoja na tenzi zingine zake k.m *Fumo Liongo, Alika kama Harusi, Wanawake wa Kiamu, Utenzi wa Mkunumbi, Utendi wa Safari* miongoni mwa nyinginezo.

Maina (2005) ameshughulikia nafasi ya mwanamke katika tenzi mbili za Shaaban Robert, utenzi wa *Hati* na utenzi wa *Adili***.** Katika kazi yake alitumia tawi la nadharia ya ufeministi ambalo linasisitiza uundaji wa jamii mpya ambayo itazingatia usawa wa wana. Pia, ameshughulikia falsafa ya mshairi Shaaban Robert kuhusu maisha. Tofauti na kazi yake tumelinganisha na kulinganua jinsi watunzi wawili Robert na Kijumwa wameshughukia swala la maadili kwa vijana wa kiume. Mhakiki Maina ameshughulikia tenzi mbili za mtunzi mmoja Shaaban ambazo ni *Hati* anapomwusia kijana wa kike na *Adili* ambao anamwusia kijana wa kiume. Kazi yake pia imetufaidi mno hasa katika marejeleo yetu kwenye utenzi wa *Adili.*

Gudrun na Vierke (2010) katika kitabu chao *Texts From the Dammann Papers and Other Collections,* wameshughulikia mkusanyiko wa kazi za Kijumwa zikiwemo barua za Kijumwa kwa Dammann, tarihi, nyimbo za mapenzi na tenzi tofautitofauti ukiwemo utenzi wa *Siraji*. Kazi yetu ni tofauti na yao kwani sisi tumejikita katika kazi moja tu ya Kijumwa ambao ni utenzi

wa *Siraji*. Hata hivyo, kazi yao imekuwa ya manufaa kwetu kwa kutupa mwongozo wa kuelewa zaidi utenzi huu wa *Siraji* na kwa kuirejelea kazi hii tumeweza kusoma kazi nyingine za mtunzi Kijumwa.

Watuha (2011) alichunguza na kubaini wazi maudhui ya waadhi katika utenzi wa *Adili* ulioandikwa na Shaaban Robert.Tofauti na kazi yake tumeshughulikia swala la maadili katika tenzi mbili, utenzi wa Kijumwa *Siraji* na utenzi wa Robert *Adili.* Aidha alielezea falsafa ya mshairi Shaaban Robert kuhusu maisha ya kijumla ulimwenguni na mtazamo wake kuhusu maisha. Kazi yake imetufaidi sana kwani alitumia nadharia ya maadili sawa na yetu hivyo tumeirejelea kila mara ili kutupa mwongozo katika kushughulikia mada yetu.

Ngunjiri (2012) ameshughulikia matumizi ya taswira kama kigezo cha kufanikisha maudhui katika utendi wa *Siraji.* Tofauti na kazi yake, tumeshughulikia maadili katika vijana wa kiume katika tenzi mbili *Siraji* na *Adili.* Mhakiki Ngunjiri alichunguza kigezo cha taswira na umuhimu wake katika kufanya maudhui ya mtunzi yawe ya kutambuliwa na kuthaminika na wasomi. Kazi yake imetufaa sana kwa sababu alishughulikia mojawapo ya tenzi ambazo tumeshughulikia *Siraji*. Hivyo basi, hatukuwa na budi kurejelea kazi yake kila mara ili kutupa mwanga zaidi.

Nyamemba (2015), amelinganisha maswala ya vijana miongoni mwa waandishi katika diwani ya *Tunu ya ushairi* ya mhariri Timothy Arege ambayo ina mkusanyiko wa mashairi ya watunzi wanne. Aliweza kushughulikia maswala mbalimbali ya vijana maadili yakiwemo. Ingawa ameshughulikia maswala ya vijana wa kike na wa kiume kwa jumla tofauti na kazi yetu tumeshughulikia vijana wa kiume tu. Kazi yake pia imekuwa ya manufaa kwetu kwani baadhi ya maswala aliyoyashughulikia yanawiana na yetu kama yale ya nidhamu na maadili mengineyo. Hivyo tumefaidika kwa kuirejelea kazi yake kupata mwongozo zaidi.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada katika kazi zingine

Katika kazi zingine kama zile za tamthilia na riwaya, wapo watafiti wameshughulikia maswala ya vijana kwa njia tofautitofauti. Wafula (1999) ameshughulikia uhakiki wa tamthilia tatu kuhusu wahusika vijana. Tamthilia hizo ni: *Wakati ukuta*, *Hatia* na *Uasi.* Katika kazi yake

ameshughulikia jinsi vijana huweza kubadilika kwa urahisi kadri imani zao za kimsingi zikijengeka. Uhakiki wake haujafafanua kiwango vijana wamefanikiwa kujikomboa kutokana na matatizo yao ya kila siku katika jamii. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na yetu kwani amejikita kwenye vijana kwa jumla nasi tumejikita kwenye vijana wa kiume. Hata hivyo, utafiti huu wa Wafula umetupa mwongozo kuelewa baadhi ya changamoto zinazowakumba vijana.

Manoti (2012) alishughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika riwaya ya *Upotevu.* Tofauti na kazi yetu, yeye alichunguza ni kwa kiasi gani dhamira ya uozo inajitokeza katika riwaya ya *Upotevu* ilhali sisi tumechunguza maadili ya vijana wa kiume katika tenzi. Kazi yake ina manufaa kwetu kwa sababu alitumia nadharia ya maadili sawa na iliyotuongoza katika utafiti wetu. Hivyo kazi yake imetufaa sana kupata mwelekeo na kuielewa zaidi nadharia hii ya maadili.

Naliaka (2012) alihakiki hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Katika utafiti wake alitilia maanani matatizo yanayowakumba vijana kwa jumla katika riwaya hii. Tofauti na kazi yake tumejikita katika maadili ya vijana wa kiume katika utenzi wa *siraji* na wa *Adili* kwa kuongozwa na nadharia ya maadili kinyume na yeye alijikita katika vijana wote kwa jumla kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia. Katika utafiti wake amebaini kwamba vijana wamekumbwa na changamoto nyingi sana ambazo zinachangiwa na ukosefu wa malezi bora na pia matatizo ya kiuchumi. Kazi yake imetufaa sana kwa sababu aliyashughulikia baadhi ya maswala ya vijana sawia na yetu hasa zile changamoto zinazowakumba vijana kutokana na ukosefu wa malezi bora. Hivyo hatukuwa na budi kuirejelea kazi yake kila mara ili kupata mwelekeo zaidi katika utafiti wetu.

Kwa maoni ya Naliaka, swala la kuzorota kwa maadili limechangiwa sana na kutowajibika kwa wazazi katika kuwaelekeza wana wao. Tumeyaunga mkono maoni ya Naliaka kwamba wazazi wengi hukosa nafasi ya kukaa na wana wao ili kuwashauri jinsi wanavyostahili kuishi. Wazazi hutumia muda mwingi katika mambo mengine hasa ya kutafuta mtaji. Kazi hizo zote tulizozitaja katika sehemu ya 1.6.1 na 1.6.2 zimechangia mno katika utafiti wetu kwani tumezirejelea mara kwa mara tunapoendelea na shughuli yetu ya utafiti.

## 1.7 Msingi wa kinadharia wa utafiti

Katika sehemu hii tumeweza kuielezea nadharia ambayo tumeitumia katika utafiti wetu na uhusiano wa nadharia hiyo na kazi yetu na hatimaye mihimili ya nadharia yenyewe ambayo imetuongoza katika utafiti mzima.

### 1.7.1 Nadharia ya maadili

Nadharia ya maadili ni nadharia kongwe ambayo iliasisiwa Ugiriki na Roma. Mwasisi wa nadharia hii ya maadili ni Plato aliyekuwa mwanafalsafa wa Kiyunani na mwanafunzi wa Socrates. Plato aliishi kati ya mwaka 427 na 345 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Plato alisisitiza kwamba lengo kuu la fasihi ni kuadilisha na isipofanya hivyo basi inafaa ipigwe marufuku. Hayo ni kwa mujibu wa Wamitila (2003). Kuna wataalamu wengine ambao baadaye walichangia katika nadharia hii ya maadili ambao ni Aristotle, Horace, Hough, Tolstoy na wengine. Nadharia hii inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kujenga jamii bora yenye maelewano kwa kuangalia kazi za kifasihi na ubinadamu na hasa maswala ya kimaadili.

Kulingana na Wamitila (2003:266-267) nadharia hii hutumiwa kuelezea usomaji na tathmini ya kazi ya kifasihi kwa kuangalia uhusiano wake wa ubinadamu na haswa maswala ya kimaadili. Wamitila anaendelea kusema kuwa katika andiko lake *The Republic*, Plato (1960) alifafanua ya kuwa ushairi hauna budi kuchunguzwa kabla ya kupitishwa ili kuchuja athari za ushairi kwa jamii hasa vijana.

Plato na wafuasi wake waliamini kuwa ushairi hauna budi kumtumikia mtu kiroho, kumnawirisha pamoja na kumpa uadilifu wa kijamii. Hivyo basi ushairi utamwelekeza anayehusika jinsi ya kuwa mwanajamii bora. Kutokana na mawazo ya Wamitila (2003), tumeweza kuelewa ya kwamba umuhimu wa fasihi hautokani tu na jinsi ya kusema bali katika kile kisemwacho.Wahakiki wanaoutumia mkabala huu huangalia fasihi kama kitu kinachohakiki maisha ya mwanadamu na anatakiwa aone namna ambavyo kazi ya mwandishi inaweza kuwa na funzo au onyo kwa msomaji wake.

Kutokana na maelezo ya Plato akirejelewa na Wamitila hapo juu tumepata kuelewa ya kwamba fasihi hutokana na uigaji wa mazingira ya mtu na pia lengo kuu la fasihi ni kuadilisha.Wafula na Kimani (2007:28) wanasema kuwa Aristotle aliyekuwa mwanafunzi wa Plato alikubaliana na fikira za mwalimu wake kuwa sanaa ni mwigo wa maisha ya binadamu. Aristotle anasisitiza kuwa fasihi huiga kiubunifu kwa kuzingatia mambo yanayoathiri maisha ya binadamu. Uigaji huu waweza ukawa wa shari au heri. Hivyo basi jamii yaweza kuangalia na kuchuja yafaayo kuigwa na kupuuza yasiyofaa. Katika msingi huu fasihi inakuwa kama kielekezo cha jamii.

Kimani na Chimerah (1999) wanasema kuwa, nadharia ya maadili inajikita katika imani isemayo kuwa wanadamu na viumbe wote hai kwa jumla, wana kitu kiitwacho tabia na hawazaliwi nayo bali hujifunza. Wataalamu hao wanaendelea kusema ya kuwa tabia ni za aina mbili: tabia mbaya na nzuri. Mtu ana uwezo wa kuwa na tabia nzuri iwapo atapata fundi angali mtoto mdogo ili afundishwe kutenganisha tabia nzuri na mbaya. Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kwani tunajua kwamba samaki hukunjwa angali mbichi. Hivyo vijana huelekezwa wakiwa wadogo ili kutahadharishwa na kuonywa kutokana na maovu mapema na kuelekezwa jinsi ya kuishi. Ndiposa tunawaona watunzi Kijumwa na Robert wanawaelekeza vijana wao wa kiume mapema kwenye tenzi za *Siraji* na *Adili.*

Plato katika kitabu chake maarufu *The Republic* anazungumzia kuhusu Jamhuri dhahania ambayo ni kielelezo bora, yenye kiongozi mwenye maadili ya juu sana. Plato anasema kuwa viongozi wanapaswa kutengwa na maovu ili wasije wakapoteza maadili. Aidha Plato anapendekeza kuwa watoto ambao wangekuwa viongozi wa Jamhuri wangelelewa katika mazingira ambamo hawangeathirika vibaya kimaadili. Tunamkosoa Plato kwa wazo hilo la kumficha kiongozi mtarajiwa kutokana na maovu. Hii ni kwa sababu kwa maoni yetu tunaona ni vyema kiongozi kuelewa ukweli wa maisha ndiposa atakapokumbana na changamoto za maovu katika jamii, aweze kukabiliana na kupambana nazo kwa ujuzi ili kupata suluhisho.

Katika maandishi yake Plato *The Republic,* anasisitiza ya kuwa ni sharti kazi ya ushairi kuchunguzwa kabla ya kupitishwa ili kuchuja athari za ushairi kwa jamii hasa vijana.

Aidha Plato anapendekeza kuwa mtunzi wa kazi ya fasihi ni sharti ayaelezee mazuri tu ya mashujaa na watawala wa nchi. Hatukubaliani na maoni hayo kwani tunaonelea kwamba ni

muhimimu kazi ya fasihi kushughulikia mambo halisia katika jamii yakiwemo maovu ili kuwakosoa wanaopotoka na kupendekeza njia mwafaka za kujiepusha na uozo katika jamii.

Watuha (2011) akimnukuu Timmons (2002) anasema kuwa, kuna aina mbili za madhumuni muhimu ya nadharia ya maadili. Nayo ni ya kiutendaji na ya kinadharia. Nadharia ya maadili ya kiutendaji inahusu utaratibu unaofuatwa ili kutambua jambo lipi ni sawa na lipi si sawa. Nadharia ya maadili ya kinadharia inahusu kiini kilichomo katika utendaji ulio sawa na usio sawa, ubaya au uzuri wa jambo. Kwa hivyo nadharia hii inalenga kuchanganua kilichomo ndani ya vitendo ambacho huvifanya vitendo hivyo kuwa sawa au kutokuwa sawa. Hata hivyo mikabala hiyo miwili inahusiana sana. Watuha anaendelea kusema ya kuwa kila jamii ina kanuni zake ambazo kwazo kitendo chaweza kuonekana sawa au si sawa. Maoni ya Timmons yanaoana na ya wataalamu wengine tuliowarejelea hapo mwanzo kwamba nadharia hii inajihusisha na utaratibu wa kuangalia na kuchunguza kazi ya kisanaa katika kuchuja yaliyo potovu na yale yaitwayo maadili katika maisha ya binadamu. Hivyo basi, ni jukumu la watu wazima katika jamii kuwapa vijana maadili ili kuwaelekeza na kuwatahadharisha maishani mwao.

Msanii maarufu Tolstoy (1960) naye alichangia katika nadharia ya maadili. Aliandika vitabu maarufu *War and Peace* na *Anna Karenina*, hadithi fupi na vitabu vingine. Anasema kuwa ujumi na uzuri wote wa sanaa hutegemea maadili ambayo hupitishwa kwa wanajamii. Vile vile alipendekeza sanaa iwe ni ya kidini ili kuelekeza watu mienendo miema ya kufuata na pia alimuunga Plato kuikashifu sanaa ambayo haikujenga maadili. Mtaalamu Tolstoy pia alichangia kwamba jukumu jingine la sanaa ni kuleta undugu miongoni mwa watu wote bila kubagua watu kulingana na matabaka. Hivyo basi kwake yeye Tolstoy dini ni muhimu sana kwa vile huleta umoja kati ya watu na watu wote ni sawa. Plato na Tolstoy waliona kwamba kupitia kazi ya sanaa wanajamii wanafaa kupata mwono wa maisha ya kimadili. Swala la maadili ni muhimu sana katika kila jamii kwani maadili huiepusha jamii na matatizo mengi na kuwawezesha wanajamii kuishi kwa utangamano.

Gitobu (2014) anasema kuwa Aristotle aliyekuwa mwanafunzi wa Plato na mwanasayansi asilia naye aliamini kuwa sanaa ni mwigo au uigaji wa maisha ya binadamu. Anaendelea kusema kuwa

uigaji huu unaweza ukawa wa shari au wa heri. Gitobu anaendelea kusema kuwa Aristotle alishikilia kuwa jamii inapaswa kuangalia na kuchuja yafaayo kuigwa na kupuuza yasiyofaa. Mhakiki Gitobu anaendelea kusema kuwa mtaalamu Horace aliyezaliwa mwaka wa 65 kabla ya Kristo aliendeleza zaidi nadharia hii ya maadili. Horace alishikilia na kuiendeleza zaidi nadharia hii. Aliyachukua mawazo ya Aristotle na kuyageuza kuwa sheria zilizopaswa kufuatwa na watunzi chipukizi. Katika makala yake Horace, *The Art of Poetry* ambayo yamenukuliwa na S.T Dorsh katika kitabu cha *Classical Literary Criticism.* Horace ametoa orodha ya baadhi ya maelekezo, miongoni mwayo ikiwa ya fasihi, ambayo yasisitiza ni lazima ilenge kuadilisha na kusisimua.

Hough (1966) aliyenukuliwa na Gitobu (2014) anasema kuwa nadharia hii ya kimaadili inasisitiza kuwa kanuni za ukamilifu wa fasihi ni sawa na kanuni za utimilifu wa maisha. Mhakiki Gitobu kama hapo juu anaendelea kusema kuwa ni kupitia fasihi ambapo jamii inapata maadili mema ya kuiga kwa kuzingatia data zilizofanyiwa uamuzi mwema wa uadilifu sawa na ambavyo maisha hufanya.

Kwa ufupi, tumeweza kupata kuwa nadharia ya maadili inahusu kiini kilichomo katika utendaji ulio sawa na usio sawa. Nadharia ya maadili inalenga kuchanganua kilichomo ndani ya vitendo ambacho huvifanya vitendo hivyo kuwa sawa au kutokuwa sawa. Ni muhimu ikumbukwe ya kwamba jamii zimulikwazo na fasihi ni nyingi sana, na zinatofautiana pakubwa katika mielemeo ya kiadili. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini ya kwamba fasihi yapaswa kuyafichua maovu yaliyoko katika jamii na kuelekeza jamii kwenye mema kwa kubainisha njia za kuyashinda maovu. Hayo ni kulingana na Wamitila (2003). Nadharia hii inashikilia kwamba, watu wote wanastahili kuwa na tabia nzuri, kwa hivyo ni wajibu wa watu wazima kuwaelekeza vijana, na kila aliye na tabia nzuri kuwarekebisha walio na tabia mbaya.

Tunaona kwamba dhima ya watunzi kama walivyopendekeza wafuasi wa nadharia ya maadili ni kuelimisha wanajamii. Hivyo basi watunzi wanafaa kutunga kazi ambazo zinanuia kuwaelekeza wanaohusika kuwa wanajamii bora. Tumeichagua nadharia ya maadili ili itusaidie kuonyesha

jinsi watunzi Kijumwa na Robert walitimiza wajibu wao wa kuelimisha na kurekebisha maovu katika jamii kupitia tungo zao za kiwosia.

Mihimili ya nadharia hii ambayo imetuongoza katika utafiti wetu ni: Kwanza, fasihi ina wajibu mkubwa wa kuadilisha jamii. Mhimili huu umetusaidia katika kukusanya data kuhusiana na jinsi watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia maadili ya vijana katika tenzi zao za *Siraji* na *Adili* kwa lengo la kuwatahadharisha na kuwaelekeza maishani. Aidha mhimili huu umetusaidia kukusanya data jinsi vijana Helewa na Adili wanavyofaa kuishi kwa uelewano kwa kufuata maadili hayo wamepewa na wazazi wao.

Pili, ni binadamu aliye na uwezo wa kuamua mkondo wa mwelekeo wa vitushi katika jamii mahususi. Kigezo hiki kimetufaa pale ambapo tumetathimini manufaa ya ujumbe wa watunzi Kijumwa na Robert kuwaelekeza vijana wao wa kiume katika jamii zao mahususi ili kujenga jamii bora na sababu za tofauti zao katika mikondo yao ya uelekezi.

Tatu, binadamu ana jukumu la kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia kwa kutenda matendo mema. Mhimili huu umetusaidia kubaini umuhimu wa matendo ya kimaadili ambapo tumepata ya kwamba kutokana na matendo ya kimaadili uhusiano bora hujengeka katika jamii na watu huishi kwa amani. Hivyo basi kila mwanajamii ana wajibu wa kutimiza katika kujenga jamii bora.

Maoni ya Wamitila (2003) ni kwamba kazi nyingi za kifasihi za Kiswahili zinaelekea kuegemezwa kwenye msingi wa kimaadili. Tunakubaliana naye kwa maoni hayo kwa sababu kuna kazi nyingi sana za kifasihi ambazo hujaribu kuwaelekeza wasomaji kuepukana na maovu katika jamii. Kando na kazi ambazo tumezishughulikia za utenzi wa *Siraji* na ule wa *Adili*, kuna kazi zingine na mfano wa kazi hizi katika tenzi ni; utenzi wa *Mwanakupona*, utenzi wa *Hati* miongoni mwa tenzi nyingine. Tenzi hizi huwaelekeza vijana wa kike jinsi ya kuishi maisha bora. Aidha kuna kazi zingine katika riwaya na tamthilia ambazo pia huwaelekeza wanajamii.
Kwa kutilia maanani mawazo hayo tumetumia nadharia hii ya maadili kuchanganua maadili yanayopatikana katika utenzi wa *Adili* wa Robert na ule wa *Siraji* wa Kijumwa. Vipengele vya

nadharia ya kimaadili vimetusaidia kubainisha mchango wa watunzi Kijumwa na Robert tukizingatia maadili miongoni mwa vijana wa kiume ili kuwatahadharisha na kuwaelekeza vijana hao.

### 1.8 Mbinu za utafiti

Katika sehemu hii tumeshughulikia njia zote zilizotumika kutambulisha data pamoja na zile zilizotumika kutathmini matokeo ya utafiti. Sehemu hii tumeigawa katika vijisehemu vitatu vifuatavyo.

#### 1.8.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli

Tumeteua sampuli lengwa katika utafiti wetu ambazo ni Utenzi wa *Siraji* wa Mohammad Kijumwa na Utenzi wa *Adili* wa Shaaban Robert. Tumeteua utenzi wa *Siraji* na ule wa *Adili* kwa sababu zina uhusiano wa karibu sana kwani tenzi hizi mbili zinahusu wasia wa wazazi wa kiume kwa vijana wa kiume. Tumehakiki tenzi hizi mbili kwa kuzisoma na kuchambua swala hili la maadili katika vijana wa kiume.

#### 1.8.2 Ukusanyaji data na mbinu za ukusanyaji data

Mbinu tulioitumia katika ukusanyaji data ni pamoja na kusoma na kuzichambua tenzi hizi mbili tulizoziteua *Siraji* na *Adili* kwa jumla. Tumedurusu kazi kadha wa kadha maktabani ambazo tumeziona zinaafikiana na uchambuzi wetu. Aidha, tumepitia tasnifu, vitabu na makala za waandishi wengine zenye manufaa kwa utafiti wetu. Vile vile, tumesoma kupitia tovuti kuhusu kazi zinazozungumzia masuala ya vijana hasa maadili na pia tumezipitia matini mbalimbali zilizoandikwa kuhusu nadharia tuliyoitumia ya maadili kisha baadaye tulilinganisha na kulinganua swala la maadili katika utenzi wa *Siraji* na wa *Adili*.

#### 1.8.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Baada ya kusoma kwa makini tenzi za *Siraji* na *Adili* ambazo tumezishughulikia na kuchambua maadili ambayo yameshughulikiwa, tumefanya tathmini yetu na kuchanganua data ambayo tumekusanya kwa njia ya maelezo na ufafanuzi huku tukitoa ushahidi kutoka kwenye matini

husika na hatimaye matokeo ya uchanganuzi wetu tumeyawasilisha kwa njia ya maelezo na ufafanuzi.

### 1.9 Muhtasari

Katika sura hii ya kwanza tumeanza na utangulizi ambapo tumeeleza dhana ya fasihi na umuhimu wake, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia ya maadili na hatimaye tumeshughulikia mbinu ambazo tulizitumia katika utafiti wetu. Katika sura ya pili tumeshughulikia dhana ya kijana, maadili, dhima ya maadili na maadili yalivyoshughulikiwa katika tenzi *Siraji* na *Adili*.

# SURA YA PILI

## DHANA YA MAADILI NA YANAYOJITOKEZA KATIKA UTENZI WA *SIRAJI* NA *ADILI*

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili dhana ya vijana, dhana ya maadili, dhima ya maadili na tumeelezea utenzi wa *Siraji* na *Adili* ingawa kwa muhtasari; kisha sehemu kubwa ya sura hii inahusu maadili mbalimbali na jinsi yamejitokeza katika utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili* huku tumeongozwa na mhimili wa nadharia ya maadili ambao unatufafanulia ya kwamba 'fasihi ina wajibu mkubwa wa kuadilisha jamii.' Hivyo basi mhimili huu umetusaidia kuchambua jinsi watunzi kijumwa na Robert wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume katika tenzi zao *Siraji* na *Adili* kwa lengo la kuwaelekeza wanajamii kwa jumla.

### 2.1 Dhana ya kijana

Maana ya dhana kijana hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kulingana na Ripoti ya Kimataifa (2011) kuhusu vijana, inatambulisha kijana kama mvulana au msichana mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 24

Nyamemba (2015) akiwanukuu Brown na Larson (2002) anasema kwamba dhana kijana ni telezi, kwepevu kwa sababu ya kutokubaliana kuhusu maumbile, tamaduni na vipindi vya wakati. Wanaainisha ujana kama kipindi cha maisha kilichoko kati ya mwongo wa pili na wa tatu katika maisha ya mtu. Kwa mujibu wa Brown na Larson, umri wa vijana ni kipindi kilichoko baina ya miaka 11 na 29. Aidha Nyamemba kama hapo juu anaendelea kurejelea tarakimu za wizara ya vijana na michezo iliyobuniwa mwaka wa 2008 akisema ya kwamba; sera ya kitaifa kuhusu vijana nchini Kenya, yamrejelea kijana kama mtu yeyote ambaye umri wake ni baina ya miaka 15 hadi 30.

Erikson (1961) anasema ya kwamba majukumu ya vijana yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jamii inavyoendelea kubadilika vilevile. Awali malezi ya vijana yalikuwa jukumu la jamii nzima kwa sababu watoto walikuwa mali ya jamii. Aidha majukumu ya vijana pia yalikuwa wazi, huku

vijana wa kiume wakiandamana na wazazi wao wa kiume waliowafunza maadili ilhali wasichana walifundishwa majukumu yao na mama zao. Wakati huo hapakuwa na changamoto nyingi kwani kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza vijana kulingana na kila jamii. Tunamuunga mkono mtaalamu Erikson kwa kuwa ni dhahiri kwamba kwa sababu moja au nyingine wazazi wa sasa hawatengi muda wa kutosha ili kuwapa watoto wao maadili ya kuwaongoza jinsi ya kuishi, ndiposa kumezuka changamoto nyingi kwa vijana.

Hivi maajuzi mwezi wa Julai 2016 kutokana na habari kwenye gazeti la *Taifa Leo* 20.6.2016, kulizuka janga la kuchomwa kwa mashule ya sekondari zaidi ya 117 na wanafunzi zaidi ya 100 walishtakiwa kote nchini Kenya kwa kosa la kusababisha hasara hiyo. Mbali na mashtaka hayo ya uteketezaji wa mashule, wanafunzi wengine walipatikana na vileo huku wakishiriki ngono kwenye gari walimokuwa wakisafiria. Kwa maoni yetu ni kwamba wazazi hawajatekeleza jukumu lao la kuwaelekeza wana wao jinsi ya kutatua shida zao na kuwatahadharisha dhidi ya tabia potovu kama hizo za uharibifu. Hivyo basi ni muhimu wazazi kutekeleza wajibu wao wa kuwafunza wana wao maadili kabla ya kuwapeleka shuleni. Kwa kufanya hivyo itasaidia walimu kusisitiza hiyo mienendo mizuri ili kuzuia kuzorota kwa maadili.

Kutokana na maoni tofautitofauti ya wataalamu hapo juu ni wazi kwamba dhana kijana ina utata mkubwa kuhusu ni umri gani ujana unaanza na unaishia. Ingawa tunashughulikia maadili ya vijana wa kiume, katika utafiti wetu tumezingatia kijana kama binadamu wa kike au wa kiume aliye kati ya umri wa miaka 15 hadi 35 kulingana na Katiba ya Kenya (2010). Huu ni umri ambao kijana anabadilika kutoka maisha ya utotoni hadi utu uzima na vijana wengi hukumbana na changamoto nyingi katika umri huu. Wasia wa Kijumwa na Robert kwa wana wao katika utenzi wa *Siraji* na *Adili* ni wa kuwaelekeza vijana kuanzia utotoni hadi utu uzima ndiposa tukajikita katika umri huu.

### 2.2 Dhana ya maadili

Kimsingi ni vigumu kutoa maana ya moja kwa moja ya dhana ya maadili. Hii ni kwa sababu neno hili lina maana pana sana kwani kila mtu na wataalamu mbalimbali wametoa fafanuzi tofautitofauti  na kila  watu waweza kuwa na maana zao .

Kulingana na Nyamemba (2015) anasema kuwa maadili ni hali ya kuwa na mwenendo mwema. Tunakubaliana naye mhakiki Nyamemba lakini hajafafanua mwenendo bora ni upi kwani kila jamii mahususi ina mielemeo tofauti ya kutambua maadili. Hivyo maadili hutofautina kutoka jamii moja hadi nyingine.

Watuha (2011) akimnukuu Gibbe (1980) anasema kuwa maadili ni wazo pana na la jumla sana linalorejelea wema na uwajibikaji wa mwanadamu. Tunakubaliana na mawazo yake ingawa tunaweza kusema kuwa maadili ni mienendo au tabia njema inayokubalika katika jamii mahususi kuwa kama sehemu ya maisha yao.

Kulingana na utafiti wetu tunakubaliana kuwa dhana maadili isitokane tu na makubaliano ya jamii fulani ilhali itokane na kila mtu binafsi na maadili hayo ni sharti yakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa vinavyozingatia usawa, haki za binadamu na amani na utulivu wa jamii hiyo na taifa kwa jumla. Hivyo tumeweza kuona kwamba maadili ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote wanaotangamana katika shughuli za kila siku ulimwenguni. Ili mtu kusemwa kuwa ana maadili lazima azingatie haki za wengine.

Kando na utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili*, kuna tenzi zingine tofautitofauti zilizotoa maadili kwa vijana mfano *Utenzi wa Mwanakupona , utenzi wa Mtu ni Utu, utenzi wa Hati na nyinginezo.* Maudhui ya kijumla ambayo yanajitokeza kwenye tenzi hizi ni msisitizo mwingi wa tabia njema, kuwa na utu, kufuata maagizo ya kidini na kudumisha asasi ya ndoa yenye furaha miongoni mwa maudhui mengine. Aidha kitabu chake Shaaban Robert (1959) *Masomo yenye Adili* ni wasia kwa binadamu wote, wachanga kwa wazee. Katika kazi zake Robert ameshughulikia vipengele mbalimbali vya maadili. mfano utu, ukweli, bidii na kazi, dini na maadili mengine.

**2.3 Dhima ya maadili**

Katika kijisehemu hiki tumeshughulikia umuhimu wa maadili kwa jumla katika jamii na taifa zima kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia yetu kuwa ni, 'binadamu aliye na uwezo wa kuamua ni mkondo wa mwelekeo wa vitushi katika jamii.' Hivyo basi maadili ambayo watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia yana jukumu kubwa la kuleta amani miongoni mwa wanajamii ikiwa yatazingatiwa. Maadili ni nyenzo muhimu katika kufanya jamii yoyote iweze kuendelea kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Sekta zote nchini zinahitaji uadilifu wa hali ya juu wa kila mwananchi ili kukuza uchumi wetu na kuishi kwa amani. Hii hutokana na ukweli kwamba maadili ni kaida zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu.

Maadili ni hatua muhimu ambayo humtambulisha binadamu ndani ya jamii yake. Katika hali ya kawaida maadili hujitokeza katika matendo, kwa vile ndicho kielelezo sahihi cha kupima maadili ya jamii fulani. Maadili yanatuelekeza katika shughuli zetu za kila siku na yanatukinga dhidi ya uharibifu; ili kuwa na maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii ni sharti mwanzo kuwe na nidhamu na maadili ya hali ya juu. Hivyo maadili ni muhimu katika ujenzi wa taifa lolote lile.

Taifa lazima lijengwe kwenye misingi ya maadili ili kuwa na maendeleo ya kiuchumi. Kwa vile maadili humwelekeza mwanadamu kutambua mema na maovu, ni lazima tujenge maadili ya familia zetu, ya vijana, taifa na ya viongozi. Aidha ni muhimu ikumbukwe ya kwamba vijana ni tegemeo la taifa la kesho, kuanguka au kuendelea kwa taifa hutegemea misingi ya kimaadili na nidhamu. Hivyo vijana lazima walelewe katika misingi ya maadili ili wajue majukumu yao binafsi, katika familia na taifa zima.

Ingawa elimu ya kawaida na sheria zina nafasi kubwa sana katika kujenga maadili ya jamii, hazitoshi kutoa mwelekeo tunaoutaka katika kubadilisha tabia za watu ili kujenga raia wema tunaowahitaji katika jamii. Hivyo ni jukumu la wazazi kujenga jamii bora kwa kuwaelekeza vijana wao kwenye maadili ili kujenga jamii bora yenye nidhamu na utaratibu kwani pasi maadili taifa lolote halitaweza kupiga hatua za kimaendeleo.

Kama vile watunzi Kijumwa na Robert walivyofanya kuwaelekeza wana wao mapema ndivyo tunaonelea kuwa msingi wa kwanza wa maadili unapatikana ndani ya familia kwani huko ndiko mtoto anakoanza kujifunza mambo na kisha kuendelea nayo katika shughuli zake hadi akiwa mtu mzima. Ndipo wahenga wakasema samaki mkunje angali mbichi. Kwa kufanya hivyo tunaongozwa na mhimilia wa nadharia ya maadili unaosisitiza ya kwamba, 'fasihi ina wajibu mkubwa wa kuadilisha jamii.' Watunzi Kijumwa na Robert wametumia mafunzo ya dini kuwadilisha wana wao ili kujenga jamii bora yenye amani. Hivyo ni muhimu wazazi kuwajibika na kuzungumza na vijana wao ili waweze kuwatayarisha kwani ndio viongozi wa kesho kama vile alivyosema Plato (1960) katika kitabu chake maarufu *The Republic*; alidai kuwa viongozi wanapaswa kuwa na maadili ya hali ya juu ili kuendeleza jamhuri ambayo ni kielelezo bora na watoto ambao wanatarajiwa kuwa viongozi wa kesho wapewa mwongozo mwema wa kimaadili ili waweze kuwa mfano kwa wanajamii wengine.

Erikson (1961) anasema kuwa majukumu ya vijana katika jamii yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jamii inavyoendelea kubadilika vilevile. Awali malezi ya vijana yalikuwa jukumu la jamii nzima kwa sababu watoto walikuwa mali ya jamii. Tunamuunga mkono mtaalamu Erikson kuwa awali hapakuwa na changamoto nyingi miongoni mwa vijana kama sasa kwani kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza kulingana na kila jamii. Ni wazi kuwa wazazi wengi siku hizi wamewaacha vijana wao huru sana kwani hakuna maadili ya kuwaelekeza ilhali wanaiga mambo yasiofaa kupitia mitandao ya kijamii. Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ongezeko kubwa la kuzorota kwa maadili hasa kwa vijana tofauti na ilivyokuwa zamani.

Maadili ya vijana wa kiume ambayo tunayashughulikia yameporomoka sana kulingana na ripoti za Umoja wa Mataifa ziliponukuliwa kwenye mtandao *Utandawazi na Maadili ya Vijana* 2015. Inaonekana kwamba baadhi ya vijana wa kiume imekuwa ni kawaida kuwaona wanatoboa masikio na kuvaa herini, wamesuka nywele, wamepaka poda na kuvaa suruali chini ya makalio. Hata nidhamu ya wanafunzi katika mashule na vyuo vya masomo imeshuka sana ndiposa tunashuhudia migomo, na uharibifu mwingi hasa wanafunzi kuchoma mabweni na mengine maovu. Haya yote ni matokeo ya utandawazi. Ingawa mitandao ina faida zake ni muhimu vijana kujihadhari kuiga mambo maovu.

Ripoti za Umoja wa Mataifa (2011) zilivyonukuliwa kwenye gazeti la *Taifa Leo* tarehe 17.10.2015 zinaonyesha kuwa vijana wengi hutumia muda mwingi sana kuchokora tovuti zinazohusiana na maovu kama yale ya kujiunga na ugaidi, matumizi ya mihadarati, mapenzi ya jinsia moja miongoni mwa maovu mengine. Hivyo ni muhimu wazazi kuwajibika kwa kuwatahadharisha vijana wao na kutowaacha vijana wao huru sana na utandawazi kwani huchangia katika kuzorota kwa maadili.

### 2.4 Maadili yanayojitokeza katika utenzi wa *Siraji*.

Katika kijisehemu hiki tumeshughulikia yale yanayohusiana na utenzi wa *Siraji* ingawa kwa muhtasari kisha tumeyachambua maadili yanayojitokeza katika utenzi huu wa *Siraji* kwa jumla. Kwa kufanya hivyo tumeongozwa na mihimili muhimu ya nadharia ya kimaadili iliyotuongoza katika utafiti wetu. Utenzi wa *Siraji* ulitungwa na mtunzi maarufu Mohammad Kijumwa mnamo mwaka 1927. Utenzi huu una beti 209 na unahusu wasia wake Mohammad kwa mwanaye wa pekee wa kiume Helewa. Mohammad Kijumwa amempa mwanaye mawaidha ambayo aliyafungamanisha na dini ya Kiislamu ili Helewa aweze kuyatumia katika maisha yake na kuyaeneza kwa wanajamii wengine. Mawaidha haya ni ya kumwelekeza anapotangamana na wanajamii wengine.

Aidha mawaidha hayo yangejenga uhusiano mwema na Mungu pia na wanajamii kwani bila Mungu hakuna aliwezalo mwanadamu katika maisha yake. Kijumwa amemshauri Helewa kuyashika mawaidha hayo na kuyatumia katika harakati zake za kila siku kuanzia akiwa kijana mdogo, atakapooa na pia akiwa mzazi. Aidha, amemshauri jinsi ya kujenga uhusiano mwema kati yake na watu wa ukoo, majirani, marafiki, masikini na matajiri bila kusahau walemavu.

Utenzi wa *Siraji* ulipewa jina ‘Siraji’ ambalo maana yake ni taa ambayo ni ishara ya mwangaza. Kazi ya taa hii ni kumulika kisha kumwongoza mtu. Utenzi huu ulitungwa kusudi kumwongoza kijana Helewa maishani mwake ili asipotoke na kukosa mwelekeo maishani. Abou (1983) amegawa dhamira ya mwandishi wa utenzi huu wa *Siraji* katika sehemu tatu kuu: uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu, uhusiano kati ya mwanadamu na familia yake na mwisho ni uhusiano

kati ya mwanadamu na jamii yake. Tunakubaliana na maoni ya mtaalamu Abou kwani mawaidha ya Kijumwa kwa kijana wake hutegemea ni wakati gani, mazingira yapi na kwa nani.

Katika kujenga uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu, Kijumwa anamshawishi mwanawe kumtegemea Mungu katika kila jambo kwa sababu kila kitu kizuri hutoka kwa Mungu. Ili kujenga familia yake Helewa amefafanuliwa majukumu yake kama mume na mzazi ili aweze kuwajibika ipasavyo. Aidha, Katika kujenga uhusiano mwema na jamii amemshauri Helewa kuwa na adabu na heshima kwa kila mmoja katika jamii. Maadili ambayo yameshughulikiwa na Kijumwa katika utenzi huu wake ni kama yafuatayo:

### 2.4.1 Dini na imani kwa Mungu

Kwa kuongozwa na nadharia yetu ya maadili tuligundua ya kwamba ujumi na uzuri wote wa sanaa hutegemea maadili ambayo hupitishwa katika jamii. Wafuasi wa nadharia hii hasa Plato akiungwa mkono na Tolstoy kama tulivyoelezea mchango wao hapo awali, walipendekeza sanaa kuwa ya kidini. Hivyo basi, imedhihirika wazi kuwa kazi ya mtunzi Kijumwa ilisawiri maadili ya kidini kwa kumshawishi mwanaye Helewa kumcha Mungu na kumtegemea katika kila jambo. Katika utenzi huu wa *Siraji* imani ya dini ya Kiislamu imesisitizwa na mtunzi ambapo amenukuu aya nyingi za *Qu'ran* kusisitiza ushauri wake. Mtunzi anamshauri mwanaye kumwogopa Mungu katika kila jambo ndipo ataokoka. Dini na imani kwa Mungu ndio mawaidha ya kwanza kabisa ambayo Kijumwa anampa mwanaye.
Tazama ubeti wa tano:

> "Kwanda baba mcha mungu,
> Utaokoka mwanangu,
> Huku huko kwa utungu
> Kukosa cha kutimia." ub.5.

Katika ubeti wa 159 tunapata ujumbe wa mtunzi ya kwamba Mola ndiye atoaye na kunyang'anya hivyo anamshauri mwanaye kumuamini Mungu kila wakati na kuwa na subira.

Aidha anmshauri asijitie shaka wala kuangaika na maisha kwani Mungu atamjalia na kumpa riziki kwa subira yake.

> “Wata na kupapatika,
> Moliwa wako kumbuka,
> Mola hupa na kupoka,
> Subiri atakwetea.” ub. 159.

Aidha Kijumwa ameonyesha msingi wa imani anapomshawishi Helewa kunyenyekea na kuomba msamaha kutoka kwa Mungu kwani Mungu humpokea yule amrudiaye. Vilevile anamshawishi kusoma aya katika *Korani* ambacho ni kitabu kitakatifu ambayo inasema ya kwamba Mungu husamehe wenye dhambi kwa vile binadamu ni kiumbe dhaifu bila shaka hukosea. Pia katika *Korani* inasema ya kwamba Mungu ndiye ayajuaye yote ambayo binadamu anayetenda hata kama ni kwa siri. Hivyo ni kheri kutubu kwa maovu tuyatendayo na Mungu atakubali kutusamehe. Tazama kwenye *Korani Takatifu* katika inasema haya:

> “Naye ndiye anayepokea toba kwa waja wake,
> na anasamehe makosa, na anayajua mnayo yatenda.” sura ya 42:25.

> “Kurani hutwambia,
> Nawe soma hiyo aya,
> Toba ukitubia,
> Toba Mungu hupokea.” ub.70

Kijumwa anapohitimisha utenzi wake katika ubeti wa 205-207, anamshawishi Helewa kuuchukua ushauri aliompa kuwa dira ya kumwongoza maishani ndiposa Mungu atambariki. Mtunzi pia anamwomba Jalali kuwakinga na aibu kila wakati ili wang’are kama taa. Hayo yote yanaonyesha wazi kwamba mtunzi anamwamini Mungu kuwa mwenye uwezo katika kila jambo na bila yeye binadamu hawezi kuyatekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha anamwomba Mungu kubariki jamii nzima ya waislamu ambapo ni thibitisho tosha kuwa Mungu ndiye tegemeo katika kila jambo.

### 2.4.2 Adabu, utii na heshima.

Mtunzi Kijumwa anasisitiza utii na unyenyekevu kwa wazazi, wakuu katika kazi na wafanyikazi

wengine. Mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika kuyafafanua mawaidha haya imeweka wazi ya kwamba ‘binadamu ana majukumu ya kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri pa kuishi.’ Hivyo basi, ni jukumu la mwana kuwa na adabu na heshima kwa wazazi ili kujenga uhusiano wake nao na kuishi kwa amani. Jambo hili la adabu, heshima na utii hujitokeza katika ubeti wa 43, 84 na 85. Ambapo Kijumwa anamshauri mwanaye kutowafanyia dhihaka na kuwacheka waliokuwa madarakani na kushushwa ila awafanyie heshima aliyowapa awali kwa vile ayajui ya kesho kwani huenda yale ayachekao leo yampate kesho.

“Ambao alotukuka
Kazinga akadhilika,
Simfanyie dhihaka,
Inuka kikutokea.” ub.42.

“Ukimwona terema,
Fanya za kwanda hishima,
Wala siteke kiyema,
Mara Mngu hukwetea.” ub. 43.

Aidha Kijumwa amesisitiza umuhimu wa kuwatii na kuwaheshimu wazazi hata wamteteshe vipi ni jambo la busara kutowatolea maneno yatakayosababisha uhazama kati yake na wao. Anamshauri kuwaheshimu watu wote ambao wana cheo na wasio na cheo, watajika na wasiotajika, mabwanyenye na wanyonge kwani kwa kufanya hivyo jamii bora yenye amani itajengeka. Ni dhahiri kuwa Kijumwa aliyafungamanisha mawaidha yake na mafunzo ya dini kwa vile kwenye *Kurani* kitabu takatifu katika mafunzo haya kuhusu adabu kwa wazazi yanajitokeza:

“…..na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifika uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata : Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa heshima.” sura ya 15: 23

Tazama beti hizi:

“Mtii baba na mama,
Hata wakikusukuma,

Inyamaze yatakoma,
Simjibu ovu moya.” ub.84.

“Ndia enda kwa adabu
Watumwa wa waarabu,
Wamkie na karibu,
Wakipita kuwaambia.” ub. 85.

### 2.4.3 Elimu

Mhimili wa nadharia ya maadili iliyotuongoza ulitubainishia kutambua kuwa ‘binadamu ni kiumbe aliye na majukumu ya kutekeleza ili kujenga jamii bora na kutafuta njia mwafaka za kutatua matatizo katika jamii.’ Hivyo basi, Mohamed Kijumwa anamshauri Helewa kuimiliki elimu kwani ina manufaa sana na huleta mabadiliko kutokana na wanajamii kutambua ni yapi mema na maovu. Ni haki ya kila mtoto kupata elimu kwani elimu ni ufunguo wa maisha. Wazazi wa Kijumwa walitimiza wajibu wao kwa kumpa elimu hasa ya dini chuoni ndiposa ikamwongoza maishani hadi kufa kwake. Historia ya mtunzi Mohamad Kijumwa inatufunulia ya kwamba mtunzi alipata masomo ya chuo ndiposa akaweza kuielewa *Qu’ran Takatifu*. Aidha alitafsiri kazi kadhaa ambazo zimeandikwa katika hati ya Kiarabu. Hayo ni kwa mujibu wa Abou (1983).

Hivyo basi, tunaona ya kuwa maisha ya mtunzi alipokulia yalikuwa ya kiusomi. Katika kazi yake kwenye utenzi huu wa *Siraji* amenukuu sura nyingi za *Qu’ran Takatifu.* Huu ni ushahidi tosha kuwa mtunzi anaienzi elimu. Vilevile Kijumwa aliwajibika kumpeleka Helewa chuoni kupata elimu ndiposa anamshauri Helewa pia kutekeleza jukumu hilo la kuwapa wanawe masomo ya chuoni ambapo watapata mwelekeo wa kutambua mema na maovu ili kutembea kwa njia inayostahili.

“Wenu wana wa chuoni,
Kabisa siwalicheni,
Wakiomba majumbani,
Kuomba watazoea.” ub.47.

### 2.4.4 Wema na utu

Mtu anapotenda mambo mema anasemekana kuwa na utu. Matendo mema huleta sifa njema kwa mtu kwani mema huwa yanakubalika katika kila jamii. Kwa kujikita katika nadharia ya maadili tumebaini ya kwamba wema hutegemea jamii mahususi ndiposa mtunzi ameyataja baadhi ya matendo mema ambayo anayatarajia mwanaye kuyatekeleza. Hivyo basi Mtunzi Kijumwa anamshauri Helewa kutenda mema kama alivyofanya nyanyake Helewa kwa jina Kamari ambaye alikuwa na sifa ya kuwashughulikia wagonjwa hata wenye harufu ya vidonda bila kuwafukiza wala kuwabagua kwa njia yoyote ile. Mfano wa matendo mema aliyoyataja mtunzi ni: kuwasaidia wagonjwa hata wale wenye vidonda na harufu bila kuwadharau, kuwapa msaada wasiobahatika katika jamii kama maskini na walemavu, akitumwa akubali na arudi upesi kumpa majibu anayemtuma, kutoitisha pesa nyingi anapofanya kazi. Hayo ni miongoni mwa mengi mema Helewa ameshauriwa na Kijumwa kuyatenda.

> “Na uchenenda ndiani,
> Ukiona masikini,
> Ulo nacho mfukoni,
> Mpe naye ngaa moya.” ub.71.

> “Kwa mamangu walikiya,
> Magonjwa yamewaneya,
> Sikuona siku moya,
> Pua akiwashikia” ub.75.

### 2.4.5 Tamaa

Mtunzi Kijumwa anamshauri mwanaye Helewa kuachana na tamaa hasa wakati wa kula; kutaka kuomba chakula kingi kupita kiwango chake na pia kuramba vidole.Vile tujuavyo tamaa ni tabia hasi ndiposa mwana anastahili kuonywa mapema dhidi ya tabia kama hiyo. Kwa kutumia nadharia ya maadili iliyotuongoza katika utafiti wetu inadhihirika kwamba fasihi inafaa kutahadharisha wanajii dhidi ya maovu ndiposa katika ubeti wa 88 Kijumwa amemtahadharisha Helewa dhidi ya kuitisha ujira mwingi katika kufanya kazi kwani hiyo huonyesha tamaa ya pesa ambayo ni tabia hasi.

Hivyo basi, ni jambo la busara mtu akifanya kazi aitekeleze ipasavyo sio tu kutegemea na malipo kwani Mungu ndiye hutoa riziki kwa wacha wake. Ni jambo la kawaida kwamba siku hizi binadamu hutafuta kazi yenye ujira mwingi ili waweze kuwa mabwanyenye na kusahau kwamba Mungu ndiye hutoa riziki hata kama ni kidogo ni heri kushukuru kuliko kulalamika. Hivyo basi mhimili wa nadharia ya maadili umetuongoza kubaini ya kwamba mwanadamu ana wajibu wa kuwajali wenzake ili jamii iweze kuendelea vyema.

"Na lingine nimekupa,
Uiziwie na pupa,
Na katiti tena nipa,
Usinene vumilia." ub.60.

Aidha katika ubeti 137 Kijumwa amemtahadharisha Helewa dhidi ya kula upesi upesi kwani anaweza kusakamwa na chakula na hii tabia humharibia jina kwani ni tabia hasi. Vile vile, mtunzi anamshauri mwanaye kufanya mambo yake kwa utaratibu kwani tujuavyo harakaharaka haina baraka na polepole ndio mwendo. Anasema haya:

"Kula upesi upesi,
Na hili huniukusi,
Fanya mambo kwa kiasi,
Mara zitakupalia." ub.137.

Hayo mawaidha ya Kijumwa kwa Helewa kuhusu tamaa yaweza kutumika kwa jamii yoyote ile kwani watu wengine hupenda kujitakia makuu na kutojali wengine. Watu hunyakua mali na kumiliki kila kitu kuwaacha wengine wakihangaika na umaskini. Hiyo tabia hasi ndio mtunzi Kijumwa anakemea.

**2.4.6 Ukarimu**

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inasema kwamba ukarimu ni kitendo cha kuwapa watu mahitaji yao. Yaani, kuwa na roho ya kusaidia. Mtunzi Kijumwa amemsisitizia mwanaye kuwa na ukarimu kwa kuwasaidia marafiki, majirani, wagonjwa na wote wasiojiweza

katika jamii bila ubaguzi. Anamshawishi kufanya ukarimu katika kusaidia maskini na matajiri, walemavu, kuwafariji walio msibani, kutoa misaada ya nguo, kuwasaidia wagonjwa, kutoa mikopo ya pesa na kutenda kila aina ya ukarimu. Vile tunajua Zaka au 'Zakat' ni mojawapo ya nguzo tano za Uislamu. Kutoa Zaka ni nguzo ya nne ya Kiislamu; na kila Muislamu akiwa na kiwango maalumu cha mali, amelazimishwa kuitoa ili kuwasaidia mafukara. *Kurani Tukufu* inasema:

*"Na Amekuutiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini vyote vimetoka kwake"* sura (45:14)

Tena anasema Mwenyezi Mungu, "*Na kama wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika dini*" sura ya (9:11).

Bila shaka kutoa Zaka kunaimarisha undugu wa Uislamu, na mwenye kuitoa tu ndiye ndugu ya Waislamu wengine. Hivyo ni wazi kwamba ushauri wa Kijumwa unaambatana na mafunzo ya dini hasa ya Uislamu. Basi katika utenzi wa *Siraji* mtunzi amesema kuhusu ukarimu ya kwamba mtu akija kuomba msaada ikiwa ni mkopo ampe na hata ikiwa ni usaidizi wa bure kwa masikini ajitahidi kutoa hata kama ni vichache. Tazama beti hizi:

"Mwendo kikuhitajiya,
Bure karidha akiya,
Mapesa nguo rupiya,
Ulichonacho ridhia." ub.23

"Na akiwa maskini,
Kwa uwezalo sikhini,
Kheri naye muawini,
Mbili tatu au moya." ub.31.

**2.4.7 Mapenzi ya dhati**

Mtunzi anamshauri mwanaye Helewa kuwa na mapenzi kwa mke wake atakapooa na pia kuwapenda watoto kwa kuwapa mahitaji yao ya kimsingi. Ni jukumu la kila mwanamume Muislamu kumpenda mke na ndugu zake hata kama humtukana hafai kuweka chuki ila

kuwasamehe na kuwaachia Mungu. Aidha mtunzi anamshauri Helewa kumpenda yeyote ampendaye kwa dhati hata kama ni mnyama kama paka na pia kuwaonyesha ndugu zake mapenzi bila kuwabagua wakubwa kwa wadogo; awaonyeshe uso wa tabasamu kila anapokutana nao ndiposa watu wote wakiona waweze kuvutiwa kwake. Mawaidha hayo yamefasiriwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa, 'mwanadamu ana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.' Hivyo mtunzi anasisitiza mapenzi ya dhati kwani anaelewa kwamba yatachangia kujenga uhusiano mwema katika jamii. Tazama beti hizi:

"Na nd uzo wapende sana,
Uteke ukiwaona,
Iwapo hukutukana,
Ifanye hukusikia." ub.38.

"Akupendao hakika,
Nawe kheri kumshika,
Iyapo kua ni paka,
Bibio aliniambia." ub.44.

### 2.4.8 Kuwa na subira

Kijumwa anamshauri mwanaye kuwa na uvumilivu na subira kwani tujuavyo subira huvuta heri. Mtunzi anasisitiza kwamba ni muhimu kuwa na uvumilivu na asilalamike ingawa maisha yanaonekana kuwa magumu. Anamwambia asubiri kila aina ya mateso hata kama ni kufungwa jela na kuugua na hatimaye kufa asilalamike kwani atapata baraka kutoka kwa mwenyezi Mungu. Mawaidha haya kuhusu subira yanathibitika kwenye *Kurani Takatifu* katika sura ya 2:153-157 ambapo inasema ya kwamba ni jambo la busara kwa kila mwanadamu kuwa na subira na kuomba Mungu kila anapopatwa na shida kwani Mungu ni mwenye rehema na hamsahau mja wake na mwenye subira hupata baraka baadaye. Tazama beti hizi:

"Subiri subira njema,
Sidumu na kulalama,
Mwishowe huya malama,
Ukilalama si dawa." ub. 58.

“Subiri kulla baa,
Kwa kufungwa na kuwaa,
Hata kuwa hutokaa,
Moliwa takulipia.” ub.59.

**2.4.9 Kuwa na ulimi mzuri**

Mtunzi Kijumwa anamshauri Helewa kuchagua maneno na kufikiria kabla ya kutamka asije akayatamka maneno ya kuudhi watu na kusababisha mzozo. Anamwonya dhidi ya ulimi mchafu kwa sababu neno likishatoka ni vigumu kuliregesha kwani hata kupigwa kwa upanga kutaisha lakini neno baya haliishi ila litakuwa linamchoma mwenzake kila anapolikumbuka. Hivyo ni jambo la busara kuyateua maneno kila wakati kabla ya kuyatamka.

“Unenapo mkarami,
Yateue ya usemi,
Majaraha ya ulimi,
Hupoi yakikuingia.” ub.67.

“Kheri neno kuteua,
La upanga litapoa,
La ulimi hukuzua,
Jaraha nimekuambia.” ub. 68.

**2.4.10 Bidii kazini**

Bidii ni hali ya kujitahidi katika jambo alifanyalo mtu. Tukizingatia mhimili wa nadharia inayotuongoza katika utafiti wetu kuwa ‘binadami ana jukumu la kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.’ tunapata ya kwamba kutokana na bidii mwanadamu hupata furaha baadaye kwani tunajua kwamba achumiaye juani hulia kivulini. Hivyo basi, mtunzi anaonelea kwamba ni heri kutia bidii maishani na kujiepusha na tabia za kutegemea wengine kwani mtegemea cha nduguye hufa masikini.

Kwake Kijumwa bidii kazini ni jambo muhimu na aliye na bidii hujitengenezea jina lake kuwa maarufu.  Aidha anamtahadharisha Helewa kuwacha uvivu asije akajuta. Anamshauri kutekeleza

kazi vizuri na kuifanya kuwa nadhifu na kutoitisha malipo ya juu baada ya kazi kwani kwa kufanya hivyo ataonyesha kuwa na tamaa ambayo itamkosesha baraka. Hivyo basi ni muhimu kuwa na bidii ili aweze kufahamika kwa sifa zake nzuri.

> "Na kazi fanya nadhifu,
> Utakuwa maarufu,
> Na ujira wa raufu,
> Na ukali kutotia." ub.88.

> "Uwate uzivu wako,
> Funga sana zitu zako,
> Sanduku na nyumba yako,
> Mara utaiyutia." ub. 95.

### 2.4.11 Ndoa

Ndoa ni makubaliano au maafikiano rasmi kati ya mume na mke ili kuwawezesha kuishi pamoja kwa ajili ya kuanza familia. Katika ubeti 169-171 mtunzi Kijumwa anamshauri kijana wake Helewa kuwa wakati wake wa kuoa utakapofika amtafute mchumba ambaye ni jamaa yake kwa vile huyo mchumba atakuwa mwenye maadili na alenge kupata mchumba wa kiwango chake ndipo jina lake zuri lizidi kutukuzwa. Aidha anamkumbusha kuwa ni wajibu wake kumfurahisha mke wake atakapooa kwa kumtimizia mahitaji yake yote ya kimsingi kwani ndio desturi ya mwanamume yeyote Muislamu. Hayo mawaidha ya mume kuwajibika anapochagua mke ni kweli yapo kwenye *Kurani Takatifu* inasema:

> "Na ardhi njema, yenye udongo wa rutuba hutoa mimea yenye
> kukua vizuri yenye uhai, idhini ya Mola mlezi wake. Na ardhi
> mbaya haitoi ila mimea michache, isiyo na faida ,tena kwa shida." sura 7:58.

Hivyo basi ni ushahidi tosha ya kwamba maadili ya mtunzi Kijumwa yamefungamanishwa na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Ujumbe muhimu katika mawaidha hayo ni kwamba wanaume wafanye uchaguzi wa mke kwa utaratibu ili kuyaendeleza maadili katika jamii na pia wawatunze wake na wana wao kwa kila namna ili ndoa kudumu. Tazama beti hizi:

"Baba wangu muoapo,
Pazengee papo hapo,
Penye nasaba ilipo,
Hapo baba tegemea." ub.169.

"Zengea mwana wa kwako,
Au wa daraja yako,
Listawi ina lako,
Na wenye kukuangalia." ub. 170.

Mawaidha mengine ambayo Kijumwa amempa kijana wake kuhusu ndoa ni ya mjadala kwani kuna vile hatukubaliani nayo wala hatujui kama ni sawa au si sawa kuiga baadhi ya ushauri anaoutoa. Kwa maoni ya Kijumwa anaonelea kuwa ni bora zaidi kuwa na mchumba wa daraja lake na pia atakapooa mke akiomba ampe talaka ampe upesi bila kusita na akija kujuta atafute mwingine. Kwa maoni yetu hili halifai. Licha ya changamoto za kila aina katika ndoa ni bora zaidi kuvumiliana katika ndoa kwani hakuna mkamilifu kwa kila jambo. Ni heri kuzungumza na kutatua matatizo katika ndoa kuliko kukimbilia talaka na kuoa mwingine.

Aidha Kijumwa anamshauri mwanamke aliyeolewa katika ubeti wa 172 kwamba mwanamume akimwambia atamwacha akubaliane naye bila kuchelewa na afanye juhudi kuachana naye bila sababu; hata kama anampenda mumewe ni heri kujizuia kuliko kuendelea kuishi naye. Anamtahadharisha kwamba asipomwacha mume mwishowe atajuta. Kwa maoni yetu huo ushauri si sawa kwani hakuna mwanadamu aliye mkamilifu ila Mungu tu basi ni kawaida mara nyingine kutokea ugomvi. Hivyo ni muhimu kuchukua muda kabla ya kufanya uamuzi katika kila jambo na maisha ya ndoa yanahitaji uvumilivu. Tazama beti hizi:

"Na siku ya kukuambia,
Niwata nawe ridhia,
Ni kheri kuitokea,
Ama utaiyutia." ub.172.

“Wetu binti sikia,
Mwanamume kikwambia,
Takuwata buraia,
Akitinda nena haya.*”* ub.174.

Aidha mtunzi anamshawishi Helewa kwamba mkewe akitoka nyumba na akimwendea kumwambia arudi, naye mke amwambie subiri au atakwenda baadaye basi asimwendee tena kwani ni kama huyo mke hampendi tena. Kwa maoni yetu hatukubaliani na mtunzi kwani mtu hupewa muda kufikiria ndivyo aweze kufanya uamuzi.

“Kipendi akikimbia,
Uchenda kumwandamia,
Akajibu nitakuja,
Hayi wata kurejea tena.” Ub.186.

**2.5 Maadili yanayojitokeza katika utenzi wa Adili**

Katika kijisehemu hiki tumeshughulikia yale yanayohusu utenzi wa *Adili* ingawa kwa muhtasari kisha tumeyachambua maadili yanavyojitokeza katika utenzi huu wa *Adili* kwa kuzingatia mihimili muhimu ya nadharia ya maadili iliyotuonza katika utafiti wetu

.

Utenzi wa *Adili* ulitungwa na mtunzi maarufu Shaaban Robert na unapatikana kwenye diwani ya *Pambo la Lugha* (1966). Utenzi huu una beti 100. Katika utenzi huu anamwusia kijana wake wa kiume Adili. Mwandishi Shaaban Robert amemwelekeza kijana wake kuwa na maadili ya kumwongoza katika maisha yake. Amemshauri kumcha mungu, kuwa na adabu na utii, kuwa na heshima kwa wazazi, kuepuka uvivu, fitina, umuhimu wa elimu, kujitunza, kuchunga wakati, uvumilivu na mapenzi ya dhati katika ndoa miongoni mwa mawaidha mengineyo. Mawaidha hayo yana jukumu muhimu la kuwatahadharisha vijana na kuwaelekeza katika jamii.

Historia ya maisha ya Shaaban Robert inaonyesha kuwa kichocheo cha kutunga utenzi huu wa *Adili* kilitokana na kifo cha Amina mkewe wa kwanza ndipo Robert akachukua jukumu la kuwa mlezi mwema wa wanawe Hati na Adili kwa kuwatungia tenzi za kuwashauri jinsi ya kuishi

maishani kwa misingi ya maadili. Maadili yaliyoshughulikiwa na mtunzi Shaaban Robert ni kama yafuatayo:

### 2.5.1 Dini na imani kwa Mungu

Mtunzi anamwambia kijana wake Adili kwamba ni muhimu sana kuishi maisha ya kumcha na kumtegemea Mungu wake kwa kila jambo. Mtunzi Robert katika kazi zake za uandishi ameyazingatia mambo mengi yaliyosisitizwa na dini haswa dini ya kiislamu na utamaduni wake. Katika riwaya ya *Utubora Mkulima* (1968) ametusawiria jumuia ya Adili ambapo amejikita katika dini. Katika uandishi wake ameathirika sana na dini ya kiislamu ndipo tunaona mtazamo wake wa kidhanifu ambao umetokana na msimamo wake kwamba Mungu ndiye tegemeo na mtu akimwamini Mungu atafanikiwa. Kutokana na kifo cha mamake Robert anaamini kuwa mamake hakufa bali alilala tu akisubiri siku ya kiama anaposema kuwa, "…la hakufa wala hakuna kitu kifacho kamwe…" (1968:62, 63) Hivyo basi huu ni ushahidi tosha ya kwamba mtunzi Robert anaamini kuweko kwa Mungu hata maisha baada ya kufa kuna hukumu akhera na maisha mazuri peponi kwa watu wema.

Aidha kulingana na mtazamo wa kidini Robert haoni haja ya kutafuta raha katika maisha haya kwani anaamini kuwa furaha kamili hupatikana peponi. Pia anaamini kuwa siku ya kiama kila mtu mwema atatuzwa kwa mema yake ilhali mwovu ataadhibiwa. Hivyo ni kutokana na imani yake ya kidini ndio ilimsukuma kuonyesha wanajamii umuhimu wa maadili. Ni wazi kwamba Robert anaamini kuwepo kwa Mungu na yote yatendakayo ni kwa ajili ya mipango ya Mungu. Katika tawasifu yake tunapata kwamba mke wake akiwa mgonjwa anamwombea dua aweze kupona na anapofariki bado ana imani kwamba Mungu hakushindwa ilhali amemchukua mke wake kwa mapenzi yake. Robert anamshauri Adili kwanza amche Mungu muumbaji wa vyote ulimwenguni kwani ni bwana wa thawabu na ni wajibu aheshimiwe. Aidha anamwambia akikosa amwombe msamaha Rabi ili kusamehewa dhambi zake.

Katika ubeti wa 10-19 Robert ametoa sifa zifuatazo za Mwenyezi Mungu: Mungu ndiye muumbaji wa vitu vyote ulimwenguni na mbingu, aliziumba nyota, mito na jangwa, milima,

bahari, hewa, wanyama, samaki wa bahari. Hayo yote huonyesha nguvu zake Mwenyezi Mungu tofauti na binadamu wa kawaida hivyo ni sharti apewe heshima.

Hatimaye katika ubeti wa 19 Robert anasema ya kwamba Mungu anayajua yote yanayotokea kwa binadamu na kila ayatendaye mema bila shaka atapata malipo mazuri na ayatendaye maovu atahukumiwa akhera. Mawaidha hayo ya Robert yanatiwa mkazo na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, 'fasihi ina jukumu muhimu la kuadilisha jamii.' Isitoshe, maadili hayo yawe ya kidini ndiposa tumebaini ya kuwa mawaidha ya Robert yanathibitika kwenye *Korani Takatifu* katika sura ya 31:11 inasema kwamba Mwenyezi Mungu ndiye ameviumba vyote ulimwenguni basi shukurani zote zimwendee kwani yeye anajua yote yatendekayo hata kwa giza ambayo mwanadamu hayajui. Tazama beti hizi:

"Kwanza mche Mungu,
Mtengeza ulimwengu,
Juu akaweka mbingu,
Nyota zituanzie." Ub. 10.

"Ajua yote kwa ghibu,
Billa kusoma kitabu,
Ni bwana wa thawabu,
Wajibu aheshimiwe." Ub.19.

Robert anapohitimisha utunzi wake wa utenzi wa *Adili* katika ubeti 93-96 anaomba aombewe Jalali amjalie amani yake na mambo yaliyo mema na matakwa yake amtimizie. Aidha anamshauri ya kwamba kila wakati atubu kwani binadamu ni kiumbe dhaifu bila shaka makosa ni kawaida yake kuyatenda. Hilo ni thibitisho tosha kuwa mtunzi anaamini kuwa Mungu yuko na mambo yote mazuri atayapata kwa kuamini Mungu. Anayasema haya:

"Mwombe daima Rabi,
Akusamehe madhambi,
Mwanadamu ni vumbi,
Makosa desturiye." Ub.26.

### 2.5.2 Heshima kwa wazazi na walimu

Robert anamwasa Adili katika utenzi wa *Adili* kuwaheshimu wazazi, waalimu na watu wote waliomshinda umri na asionyeshe dharau ila awape staha. Anamwambia ya kwamba wazazi wanafaa waenziwe na watendewe mambo yote mazuri. Ni dhahiri ya kwamba Robert pia kama mtunzi Kijumwa aliyafungamanisha mawaidha yake na mafunzo ya dini. Kama hapo awali tumeshughulikia aya ya *Kurani Takatifu* katika sura ya 17:23-24 inasema kwamba ni sheria ya kila mtu kuwaheshimu wazazi na kutowakemea kwa jambo lolote lile ila kunyenyekea kwao na kunena kwao kwa heshima na kuwaombea Mola awarehemu kwa kazi ngumu wanayofanya ya kulea. Mawaidha hayo yameoana na mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa, 'fasihi ina wajibu muhimu wa kuadilisha jamii.' Hivyo basi mtunzi Robert anasisitiza heshima ili kujenga jamii bora. Tazama ubeti huu:

> "Tatu baba na mama,
> Wataka taadhima,
> Na kila lilo jema,
> Ukiweza watendee." Ub 36.

Mtunzi anamshawishi Adili achunge sana kusiwe na mvutano kati yake na wazazi kwani huenda mzozo huo ukamkosesha amani na wazazi na hatimaye kukosa baraka kwa Mungu. Aidha amemkumbusha ya kwamba baba mzazi ndiye alimzaa pasi yeye hangekuwa hai hivyo basi anafaa kumpa heshima na kumtendea mema kadri ya uwezo wake. Vilevile, mama mzazi apewe heshima kwa malezi aliyompa hadi kumfikisha aliko hivyo haki yake mama kupewa heshima bila kukemewa kwa jambo lolote. Mawaidha hayo yanawiana na yale ya mtunzi Kijumwa ambapo tulitoa ushahidi kutoka sura ya *Kurani Takatifu* 31:14 ya kwamba ni sharti kuwaheshimu wazazi. Hivyo basi haya mawaidha sawia na ya Kijumwa yamefungamanishwa na dini. Tazama beti hizi:

> "Chunga pasimee gugu,
> Kati yenu ya vurugu,
> Baba yako ni mbegu,
> Uliyochipuka wewe" ub.37.

“Mama amefanya kazi,
Katika wako uzazi,
Yakupasa kumuenzi,
Hata upate radhiya.” Ub.38.

Robert anamshawishi Adili awe na heshima kwa waalimu ambao wana jukumu kubwa la kumwondoa ujingani na kumpa elimu ambayo ni ufunguo wa maisha hivyo ana hisa ya kumheshimu. Pia Robert anamshauri Adili kujenga uhusiano mwema na waalimu wake kwa kunyenyekea kwao ndiposa kupata mwongozo mwema maishani. Ushauri huu umefasiriwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, ‘ni binadamu aliye na uwezo wa kuamua mkondo wa mwelekeo wa vitushi kwa kuyafuata yaliyo mema na kuacha maovu.’ Hivyo basi ni jukumu lake Adili kuamua kuwapa heshima walimu wake ili kufaidika. Tazama ubeti huu:

“Kadhalika mwalimu,
Mkuza yako fahamu,
Naye ana sehemu,
Heshimayo apewe.” Ub.54.

Hivyo, mtunzi Robert ameonelea ni heri jamii isisitiziwe kuendelea kuwa na heshima ambayo ni muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Mawaidha hayo yanaoana na mhimili wa nadharia ya maadili iliyotuongoza kuwa ‘binadamu ana jukumu la kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia’ Tunapata kuwa furaha hii itatokana na kuwajibika kwa kila mmoja kumheshimu mwenzake ili kutangamana kwa amani.

**2.5.3 Adabu na utii**

Robert katika utenzi wake wa *Adili* amempa kijana wake Adili maagizo ya kutii viongozi wa kiume na wa kike pia kwa kuyatekeleza yale viongozi hao humuuliza kuyafanya kwa kuwa matokeo ya adabu ni mazuri. Anamhimiza ya kwamba kila wakati awe na adabu ili aweze kupata baraka. Lengo kuu la mtunzi Robert hapa ni kutilia mkazo uzingativu wa matendo mema ili wanajamii kutangamana kwa amani. Mawazo haya yanaongozwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa ‘fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii.’ Tazama beti hizi:

"Pili tii mfalme ,
Wa kike na wa kiume,
Bila ya kinyume,
Utii uwatendee."ub.34.

"Ambatana na adabu,
Uwe nayo karibu,
Ina mazao ajabu,
Shika usiache." Ub.46.

### 2.5.4 Umuhimu wa elimu

Robert anamwambia Adili kuwa elimu ni bora kwa kila kijana kwani ndio mwangaza wa maisha. Katika utenzi wa *Adili* Robert anamwambia Adili kwamba elimu ina mwanga maishani na maisha bila elimu hayamfai mwanadamu kwani maisha ni magumu ni sharti aitilie elimu maanani ili ije kumsadia katika siku zijazo. Vilevile, elimu itamsaidia kutenganisha mazuri na mabaya. Anasema haya:

"Tano lililo adhimu,
Ni kujifunza elimu,
Ina mwanga maalumu,
Elimu kwa 'elewaye." Ub. 48.

Aidha katika utenzi wa *Hati* Robert pia amesisitiza umuhimu wa elimu kuwa humsaidia mtu kufahamu mema na maovu ili bila shaka kufuata kwa njia ipasayo. Tazama beti zifuatazo:

"Jifunze na elimu,
Uwe mtu mtaalam,
Halali na haramu.
Uweze kupambanua" ub. 30.

"Elimu kitu kizuri,
Kuwa nayo ni fahari,
Sababu humshauri,
Mtu la kutumia." Ub.31.

### 2.5.5 Bidii kwa kazi

Robert ni mtunzi maarufu aliyejulikana kwa bidii yake. Aliweza kuandika vitabu zaidi ya ishirini na umaarufu wa kazi zake ni ushahidi tosha kuwa ni mfanyikazi bora. Katika tawasifu yake *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1967) tumepata kuwa kazini mwake Robert alitumiwa kama mfano kwa wafanyakazi wenzake kwani jina lake lilikuwa maarufu na alipendwa na hata wazungu kwa uadilifu wake uliompelekea kupandishwa cheo. Katika utenzi wa *Adili* Mtunzi anamwonya mwanaye dhidi ya uzembe kuwa huleta umasikini na awe mwangalifu kwa kazi yake na kuinadhifisha ili kujenga sifa yake kuwa nzuri.Tazama beti hizi:

"Raha ya uvivu mbaya,
Umaskini huzaa,
Acha kuikaribia,
Usisikie witowe" ub. 89.

"Kazi yako idhibiti,
Ipe jicho la dhati,
Ukitoka katikati,
Wa'muzi jina wachie." Ub. 90.

Isitoshe, katika utenzi wa *Hati*, Robert anamwasa bintiye aweze kujitahidi na kufanya kazi kwa bidii ili aweze kujikimu maishani. Anamshawishi asiwe wa kutegemea wengine au mambo kutendeka kibahati ila ayafanye mwenyewe na asingoje kutendewa. Afanye bidii mwenyewe kwani akingojangoja atakuja kuchelewa na kupoteza muda. Aidha anahimiza matumizi bora ya wakati na kutokuwa na uzembe kazini kwani uvivu ni adui wa maendeleo. Mawaidha hayo yamefasiriwa kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa 'binadamu ana wajibu wa kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.' Kwa kutia bidii katika kila jambo mtu alifanyalo baadaye huvuna mema na kuishi kwa raha. Anasema haya:

"Kutumika ni sharti,
Wajibu kila binti,
Usingoje bahati,
Yote kutende." Ub. 44.

### 2.5.6 Nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii

Tunapozingatia mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa 'binadamu ana jukumu la kufanya ulimwengu kuwa mahala pa kufurahia.' Tunapata ya kwamba binadamu hukosa furaha kwa kutowajibika kuzingatia yale anayositahili kuyatenda ndiposa mtunzi Robert hakuchelewa kuyaweka wazi majukumu ya vijana wao katika utenzi wa *Hati* na *Adili* ndiposa wayafuate mawaidha hayo na kuishi kwa furaha. Katika utenzi wa *Adili* Robert anamwelekeza mwanaye wa kiume Adili kuwajibika kumpenda mkewe na watoto pia awatimizie mahitaji yao ya kimsingi. Aidha, anamkumbusha kuwafunza watoto wake maadili ambayo ni muhimu kabla ya kuwapa mali vile alivyofanyiwa na babake Robert.

Tunapata ya kwamba mtunzi Robert anadhihirisha lengo la kuwahimiza watu kuwa na ndoa thabiti yenye msingi wa dini ndiposa anamkumbusha Adili kwamba mke ndiye mama wa watoto basi ni wa maana sana. Haya yanathibitika kwenye *Kurani Takatifu* katika sura ya 31:14 ambapo watoto wanahimizwa kuwaheshimu mama kwa kazi ngumu ya malezi. Kwake yeye Robert maadili ni muhimu sana kuliko fedha ndiposa amewatungia wanawe tenzi za mawaidha ili kuwaelekeza jinsi ya kuishi. Adili pia alihimizwa na babake mzazi kwamba kabla ya kutoa ahadi ni wajibu wake aweze kuipima na akiitoa ahadi hiyo ang'ang'ane ili aweze kuitimiza kwani inabadilisha bahati. Tazama beti hizi:

> "Wafunze taamuli,
> Kila namna adili,
> Kabla kuwapa mali,
> Watoto watumie." Ub. 64

> "Na ukiweka ahadi,
> Kutimiza jitahidi,
> Inabatilisha sudi,
> Ahadi kwa avunjaye." Ub. 78.

Katika utenzi wa *Hati* amemfafanulia mwanaye msichana majukumu yake kuwa anapaswa kuwa mtiifu, msafi, mvumilivu katika ndoa, mpole na makini katika maneno ayatamkayo yasiwe na

athari mbaya kwa jamii. Kwake Robert mwanamke anapaswa kutunza mwili, moyo na akili yake, ili visije vikaingiliwa na mawazo potofu ambayo yatadhoofisha mapatano katika ndoa.

**2.5.7 Ndoa na mapenzi ya dhati kwa watu**

Ndoa ni kuungana kwa mke na mume kwa makubaliano ya kuishi pamoja. Mtunzi anamshawishi Adili kuwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe na watoto pamoja na watu wote kwa jumla. Aidha Mtunzi Robert anamshauri mwanaye kumpa heshima mkewe kama afanyavyo kwa mama mzazi kwani mkewe ni mama wa watoto wake. Pia, Adili anastahili kuwapenda watoto wake na kuwatendea mema kadri awezavyo ili hasa kuwapa mawaidha ya kuwaadilisha ili kuwafaidisha katika maisha yajayo.  Mawaidha hayo yako katika ubeti wa 59, 62, 63, 66 na 76. Tazama beti hizi:

"Sita ukioa mke,
Kwa mapenzi mshike,
Simfanyie makeke,
Ila akuanze yeye." ub. 59.

"Watoto wako wapende,
Katika moyo wagande,
Na uwezalo litende,
Liwafae baadaye." ub. 63.

Fauka ya hayo, Robert anamshauri Adili kuwa mapenzi kwa ndugu zake pia ni muhimu sana ili kujenga uhusiano mwema katika familia na  jamii kwa jumla.Vilevile, anamwaambia ya kwamba awafurahikie watu wote bila kubagua; ndugu na wana wao na kwa kufanya hivyo atawavutia walio mbali na kuwaleta pamoja kisha kuchangia jina lake kuwa maarufu. Tazama beti hizi:

"Ndugu wapende sana,
Wapendezwe kukuona,
Binti zao na wana,
Wote wakufurahie." ub. 66.

"Penda na watu wote,

Aliye mbali mvute,
Ila kuamini wote,
Hili sana liambae." ub.76

### 2.5.8 Utu wema na matendo mazuri

Utu ni hali ya kuwa na tabia nzuri. Mtunzi Robert kwa uandishi wake ameonyesha umuhimu wa utu sio tu katika utenzi wa *Adili* bali katika utenzi *Hati* na katika kazi zake nyingine kwa mfano *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1967), *Utubora Mkulima* (1968) *na Masomo yenye Adili* (1959), miongoni mwa kazi zake nyingine. Kwenye hizo kazi zake zote ameonyesha umuhimu wa utu.

Katika kazi yake ya *Maisha yangu na baada ya Miaka Hamsini* (1967), Robert ameonyesha hali ya utii na unyenyekevu kwa wakuu wa kazi na hata wafanyakazi wenzake. Yeye mwenyewe ni kielelezo cha mtu mwema anapotuambia kwamba mara zote alijidunisha na kujishusha na kuacha watu waseme kuhusu uzuri na ubora wake. Robert uk 43 na 45. Hivyo anaifundisha jamii kuwa na utu ili kujiendeleza maishani. Robert anasema kuwa wema hushinda ubaya. Anasema haya:

> "Utu ulikuwa jambo la aushi lililohusu wanadamu wote, na kanuni ilikuwa tabia ya milele, haikufa, haifi wala haitakufa."uk 100.

Katika utenzi wa *Adili* ubeti 63 anamsisitizia Adili kuwa na adabu wakati wote kwani itazaa mafanikio mengi. Tumamuunga mkono mtunzi Robert kwa mawaidha hayo kwani ni ukweli ya kwamba mtu akiwa na adabu wakati wote uheshimika na jina lake kuwa maarufu kisha kufanikiwa maishani.Wazo hilo linatiwa mkazo na mhimili wa nadhariaya maadili iliyotuongoza kuwa, 'fasihi ina jukumu la kuadilisha jamii.' Lengo la mtunzi Robert ni kusisitiza umuhimu wa matendo ya adabu katika maisha ya mtu. Mtunzi anasema haya:

"Ambatana na adabu,
Uwe nayo karibu,
Ina mazao ajabu
Shika usiachie." ub.63.

Katika riwaya yake *Utubora Mkulima* (1968), Shaaban Robert anamsawiri mhusika wake Utubora kama kielelezo cha mtu mwenye utu na tabia nzuri maishani. Utubora alijali utu wake zaidi kuliko mali na utukufu ndiposa tunamwona akiacha kazi ya mshahara mkubwa mjini na kuhamia mashambani ambapo aliendeleza uhusiano mwema na watu wa mashamba kisha kumuoa Radhia ambaye alimpenda Utubora kutokana na wingi wa utu wake.

### 2.5.9 Kuwa na ulimi mzuri

Robert anamshauri Adili achunge maneno ayatamkayo yasiwe na athari mbaya katika jamii. Asiseme mambo ya kuwaudhi watu bila sababu, aweze kunena mema na ajihadhari na kutumia lugha mbaya kwani yaweza kuleta ghadhabu kisha hasara. Hivyo basi ni jukumu lake Adili kuyachunguza maneno kabla ya kutamka kwani tunajua ya kwamba maneno mabaya huchoma na hayawezi kurudishwa kinywani baada ya kutamkwa. Ushauri huo umefasiriwa kwa kujikita kwemye mhimili wa nadharia ya maadili iliyotuongoza kuwa ‘ni binadamu aliye na uwezo wa kuamua mkondo wa vitushi.’ Hivyo basi kwake Robert anaonelea kwamba ni heri Adili kuyachagua maneno ayatamkayo ayafikiria ikiwa ni ya kujenga au kubomoa jamii. Lengo kuu la mtunzi ni kusisitiza matendo mema ya kujenga jamii bora. Tazama beti hizi:

> “Nne fanya taaluma,
> Kujifunza kusema,
> Neno linalochoma,
> Bila udhuru usitoe.” ub.40.
>
> ‘Lugha mbaya hasara,
> Inawakisha hasira,
> Na kuleta madhara,
> Hiyo yache pekee.” ub. 44

Kwa ufupi ujumbe wa maadili katika utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili* unawafaa vijana wa kiume katika jamii yoyote ile. Tenzi hizi zina uhusiano wa karibu sana kwani zote zinashughulikia maadili kwa vijana wa kiume kutoka kwa wazazi wa kiume. Kwa hakika tenzi hizi za watunzi Kijumwa na Robert zinabainisha kuwa watunzi hawa wanaelewa umuhimu wa

maadili na yeyote atakayeyazingatia atafurahia maisha yake ulimwenguni. Watunzi hao wanawasisitizia wana wao kufuata mawaidha waliowapa ili kujiepusha na maovu. Mawazo hayo yamefasiriwa na mhimili wa nadharia ya maadili iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, 'fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii.'

**2.6 Hitimisho**

Katika sura hii ya pili, tumejadili dhana ya vijana, dhana ya maadili, dhima ya maadili na maadili kama yalivyoshughulikiwa katika utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili*. Katika sura ya tatu tumelinganisha maadili yanayowiana katika utenzi wa *Siraji* na *Adili*.

# SURA YA TATU

# JINSI WATUNZI WA TENZI *SIRAJI NA ADILI* WANAVYOWIANA NA SABABU ZA KUWIANA KWAO

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii ya tatu tumechambua jinsi watunzi wa utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili* wanavyowiana katika kushughulikia swala la maadili ya vijana wa kiume na hatimaye tumebainisha sababu za kuwiana kwao. Tumeyachanganua maadili hayo moja baada ya nyingine kwa kuongozwa na mihimili muhimu ya nadharia ya maadili iliyotuongoza katika utafiti wetu ili kubaini kuwa watunzi Kijumwa na Robert wameyakuza maadili kupitia utunzi wao. Utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili* zina uhusiano wa karibu sana kwani watunzi wa tenzi hizi Kijumwa na Robert wote ni wazazi wa kiume wanaothamini mafunzo ya kimaadili ya dini ya Kiislamu ndiposa  wametoa wasia kwa vijana wao wa kiume Helewa na Adili. Wametoa onyo, ushauri na mwelekeo kwa wana wao wa kiume kupitia utunzi wao ili kuwawezesha kuwa na maadili mema maishani mwao. Hivyo basi, katika sura hii tumeshughulikia jinsi watunzi Kijumwa na Robert wamefanana katika shughuli yao ya kuwaadilisha wana wao na jamii nzima kwa jumla.

## 3.1 Maadili yanayowiana katika tenzi *Siraji* na *Adili*

Katika kijisehemu hiki tumeyachambua maadili ambayo yanawiana katika utenzi *Siraji* na utenzi *Adili*. Maadili ambayo tumeyashughulikia ni pamoja na: dini na Mungu, elimu, ndoa na mapenzi, bidii kazini, uwajibikaji, umakinifu, heshima na adabu, hasira, utu wema na matendo mema, kuweka siri, malezi bora, ushirikiano na uhusiano mwema, msamaha pamoja na kuwa na upole.

### 3.1.1 Dini na imani kwa Mungu

Watunzi Kijumwa na Robert wamewiana kwa jinsi walivyotoa wasia kwa wana wao kuhusu imani kwa Mungu. Watunzi hao wote wamewashawishi wana wao kumcha Mungu kila wakati na kuamini Mungu katika kila jambo. Watunzi Kijumwa na Robert ni wafuasi wa dini ya Kiislamu hivyo wanafanana kwa jinsi wameyatoa mawaidha yao ambapo wamejikita kwenye mafunzo ya dini. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba maoni ya wafuasi wa nadharia ya maadili tunayoitumia katika kuchambua kazi zetu hasa Tolstoy ya kwamba maadili yawe ya kidini

yamethibitika kwenye kazi za Kijumwa na Robert. Katika utenzi wa *Siraji* Kijumwa amenukuu aya nyingi za *Quran* ili kusisitiza ushauri wake kwa mwanaye.

Naye Robert katika utenzi wake wa *Adili* ameyazingatia mambo mengi yaliyosisitizwa na dini ya kiislamu na utamaduni wake na ameonyesha msimamo wake kwamba Mungu ndiye tegemeo katika kila jambo. Ni kutokana na imani yake ya kidini ndio alipata msukumo wake wa kutoa ushauri kuhusu umuhimu wa maadili. Robert amemshauri kijana wake Adili kwamba mwanzo wa mambo yote amche Mungu muumbaji ili aweze kupata thawabu. Aidha amemsisitizia kumwomba Mungu msamaha wa dhambi zake ili aweze kusamehewa kwa sababu ni kiumbe dhalili ambaye hukosea mara kwa mara. Anasema haya:

> "Mwombe daima Rabi,
> Akusamehe madhambi,
> Mwanadamu ni vumbi,
> Makosa desturiye." ub. 26.

Katika kuhitimisha utenzi wake wa *Adili*, Robert anaomba aombewe Mungu ampe furaha yake, umri mrefu na amjalie mambo yaliyo mazuri. Katika ubeti 96 anasema aombewe Mungu maisha na afya nzuri na aidha maisha yake yakiisha ulimwenguni apate uzima wa milele. Hili ni thibitisho tosha kuwa Robert anaamini kuwa Mungu yuko na ndiye huruzuku vyote mwanadamu anavyohitaji na kuna maisha baada ya kifo ndivyo anaomba atiwe peponi baada ya kufa. Tazama beti hizi:

> "Kama mwaona adili,
> Kuweka yastahili,
> Niombeeni Jalali,
> Amani yake nipewe." ub.93.

“Niombeeni maisha,
Afya kuninadhifisha,
Umri wangu ukisha,
Peponi name nitiwe.” ub.96

Mohammad Kijumwa naye sawia na Robert, anapohitimisha utenzi wake wa *Siraji* anawashauri vijana kushika wasia wake na kutenda yanayostahili na Mungu atawabariki. Katika ubeti wa 206 pia anamwambia Helewa na wenzake wang’are kama taa kwa kufuata mwongozo aliowapa ndivyo Mungu atawalipa. Hivyo ni wazi kwamba mtunzi Kijumwa anaamini kwamba Mungu huwalipa kwa kuwabariki watendao mema. Aidha katika ubeti 207 anaombea jamii ya waislamu kwa jumla waweze kubarikiwa na Mungu kuonyesha kwamba yeye mwenyewe ana maadili kwa kuwajali wenzake na kuwaweka moyoni ndiposa anawaombea wapate mema maishani.
Kijumwa anasema haya:

“Mshike wasia wangu,
Nimezowambia wanangu,
Tawabarikia Mungu,
Hini ni dira safiria.” ub.205

“Utuvishe ya stara,
Mungu kando midirara,
Kama taa mking’ara,
Ilahi tawajaalia.” ub. 206

Watunzi Mohammad Kijumwa na Shaaban Robert wamewiana kwa kumja Mungu. Mawaidha ya kwanza kabisa wamewapa ni kumja Mungu hivyo kuonyesha heshima waliyonayo kwa Mungu. Ushahidi huu upo katika ubeti wa tano kwenye utenzi *Siraji.*

“Kwanda baba mcha Mungu,
Utaokoka mwanangu,
Huku huko kwa itungo,
Kukosa cha kutumia.” ub.5

Aidha katika utenzi wa *Adili* ubeti wa kumi Robert sawia na Kijumwa anamshauri Adili kumtegemea Mungu muumbaji wa vyote. Anasema haya.

“Kwanza mche Mungu,
Mtengeza ulimwengu,
Juu akaweka mbingu,
Nyota zituangazie.” ub. 10.

**3. 1.2 Elimu**

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni au kutolewa na wanajamii. Kupitia mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa ‘binadamu ana jukumu la kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia,’ tumebaini ya kwamba bila masomo bila shaka mwanadamu hawezi kufurahi maishani kwani elimu ni kipengele muhimu kinachomwezesha mwanadamu kutambua mema na maovu. Aidha kutokana na ujuzi apatao mwanadamu kutokana na elimu humwezesha kujikimu maishani kwa kupata mahitaji yake ya kimsingi. Watunzi Kijumwa na Robert wote wameshughulikia swala hili la elimu kuwa la muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Robert anamshauri mwanaye Adili kwamba elimu ni muhimu sana kwani hutoa mwangaza kwa kila kijana na maisha bila elimu hayamfai mwanadamu na ni magumu. Hivyo anamshawishi Adili kuwa na elimu ambayo itamsaidia maishani.

Katika utenzi wa *Adili* tunayapata haya:

“Tano lililo adhimu,
Ni kujifunza elimu,
Ina mwanga maalumu,
Elimu kwa ‘elewaye” ub. 48.

Katika utenzi wa *Siraji* elimu ya chuoni / Madrassa imesisitizwa sana kwa sababu tunaona mtunzi amenukuu sura nyingi sana kila mara anaposisitiza mawaidha yake kwa Helewa. Hili ni thibitisho kwamba ni muhimu kila kijana kupata elimu chuoni ili aweze kusoma *Qu’rani* takatifu na kuyaelewa maadili ipasavyo na kuyafuata kwani maadili hayo ya Kijumwa yamefungamanishwa na mafunzo ya dini. Aidha mtunzi Kijumwa anamwusia Helewa kwamba asiwaache wanawe wa chuo wakiomba majumbani ili wasije wakazoea tabia hiyo hasi. Huu ujumbe unatuonyesha kwamba Helewa akiwa mzazi ana wajibu wa kuwapeleka wanawe chuoni ili kupata elimu ya kuwaongoza maishani na kuwafunza tabia ambazo zinastahili. Aidha kwa kupata elimu ya nyumbani na chuoni, Kijumwa anakemea tabia za wana kuombaomba; ni

muhimu wahimizwe kufanya bidii ili waweza kupata mahitaji yao bila kutegemea usaidizi kwa watu wengine. Anasema haya:

> “Wenu wana wa chuo,
> Kabisha siwalicheni,
> Wakiomba majumbani’
> Kuomba watazoea.” ub. 47

### 3.1.3 Ndoa na mapenzi

Ndoa ni unyumba au makubaliano rasmi ya mume na mke kuishi pamoja ili kuanza familia yao ilhali mapenzi ni mahaba yaani hali ya kuwa na hisia ya upendo moyoni na kumthamini mtu zaidi ya wengine. Mapenzi ndio kigezo kinachowaleta pamoja wawili wasio na uhusiano wa kidamu kuishi pamoja kama mume na mke. Watunzi Kijumwa na Robert wana maoni sawia kuhusu ndoa. Kwao wawili ndoa ni muhimu na baada ya kuoa vijana wa kiume wanastahili kuwapenda wake zao na watoto na pia kuwatimizia mahitaji yao ya kimsingi. Katika utenzi wa *Siraji* Kijumwa anasema haya:

> “Mke wako mpumbaze,
> Kwa uwezalo mweneze,
> Na wewe simteleze,
> Nde ukalimatia” ub. 177.

Katika utenzi wa *Adili* sawia na Kijumwa, Robert naye katika ubeti wa 59, 62 na 63 hakuchelewa kumshauri mwanaye wa kiume kuwapa mke na watoto mapenzi ya dhati. Anamshauri kumheshimu mke wake kama anavyomheshimu mzazi aliye mzaa yeye wala asimteteshe ila mke aanze mzozo kwa sababu mke pia atamzalia watoto hivyo ni sharti awajibike kumpenda na kumheshimu. Mawaidha haya ni kweli kwamba yamefungamanishwa na dini kwani katika *Kurani Takatifu* kwenye sura ya 31:14 inasema ya kwamba asiyemheshimu na kumtii mama mzazi kwa kazi ngumu aliyoifanya ya kubeba mimba yake na kumlea basi hawezi kuingia peponi. Aidha anamshauri kuwapenda watoto wake kwa roho yake na kuwatendea mema kadri ya uwezo wake kuwalea na kuwapa mwelekeo maishani. Anasema haya katika beti hizi:

> “Sita ukioa mke,
> Kwa mapenzi mshike,
> Simfanyie makeke,

Ila akuanze yeye." ub.59.

"Watoto wapende sana,
Katika moyo wagande,
Na uwezalo litende,
Liwafae baadaye." ub. 63

### 3.1.4 Bidii kazini

Bidii ni hali ya kuwa na jitihada unapofanya jambo. Kwa watunzi Kijumwa na Robert, bidii kazini ni jambo muhimu sana. Watunzi Kijumwa na Robert wote wamelishughulikia swala la bidii na wameweza kuukemea uzembe kwa hali ya juu sana. Katika utenzi wa *Siraji* Kijumwa anamshauri Helewa kufanya kazi safi na kwa bidii ili aweze kujitengenezea jina lake kuwa maarufu. Aidha mtunzi Kijumwa amemwonya mwanaye dhidi ya kufanya kazi kwa kuitisha ujira mwingi. Hiyo si haki kwani Mungu ndiye atoaye riziki kwa waja wake hivyo hakuna haja ya kuwa na tamaa ya pesa ila ni jambo la busara kushukuru Mola kwa kila kidogo apatacho.

Tunamuunga mkono mtunzi Kijumwa kwa mawaidha hayo kwani ni dhahiri kwamba watu wengi huwa maarufu kwa sababu ya bidii yao ambayo huwaletea sifa nzuri ya kutambulika na kila mmoja. Pia, anamtahadharisha dhidi ya kuacha vitu vyake ovyo kwani vinaweza kuvamiwa na waovu. Hivyo ni muhimu afanye bidii kuweka vitu vyake vizuri ili asije kujuta baadaye. Tazama ubeti wa 88 Anasema haya:

"Na kazi fanya nadhifu,
Uakuwa maarufu,
Na ujira wa raifu,
Na ukali kutotia." Ub. 88.

Robert sawia na Kijumwa katika ubeti 89 na 90, anamhimiza mwanaye kufanya kazi kwa bidii na amemshauri kuhusu umuhimu wa matumizi bora ya wakati. Aidha anamwonya Adili kutokuwa na uzembe kazini kwani uzembe ni adui wa maendeleo. Anamwambia ya kwamba kazi yake aifanye kwa kwa bidii na awe makini nayo ili kuimarisha jina lake. Tunakubaliana na maoni ya Robert kwa sababu mara nyingi sana tumeshuhudia kwamba watu wazembe hawafanikiwi maishani kwani huishia kufa masikini au kutafuta vya bwerere kwa kujiunga na

makundi maovu kama yale ya ujambazi na kisha baadaye kuuawa au kujipata kwenye mikono ya sheria. Hiyo tabia hasi ndio mtunzi Robert anaikemea kwa mwanaye. Katika utenzi wa *Adili* haya yanajitokeza kuhusu uvivu:

> "Raha ya uvivu mbaya,
> Umaskini huzaa,
> Acha kuikaribia,
> Usisikie witowe." ub. 89.

**3.1.5 Uwajibikaji**

Uwajibikaji ni mojawapo ya maadili muhimu ambayo watunzi Kijumwa na Robert wameshughulikia katika tenzi zao *Siraji* na *Adili*. Katika utafiti wetu tumelichukulia neno wajibu kwa maana ya jukumu ambalo ni sharti mtu kulitimiza au kulifanya. Ili mtu kuwajibika hana budi kuyachukulia majukumu yake kwa makini na awe kielelezo cha uadilifu katika jamii. Ushauri wa mtunzi kuhusu uwajibikaji umeongozwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa, 'mwanamu ana wajibu wa kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.'

Watunzi Kijumwa na Robert wanawiana sana wanavyoshughulikia swala hili la uwajibikaji. Wote wanawashauri wana wao kuwajibika katika kuzingatia wasia wanaowapa bila kufanya hivyo watakuja kujuta siku zijazo. Tenzi za *Siraji* na *Adili* ni wasia kutoka kwa wazazi wa kiume kwa wana wao wa kiume Helewa na Adili. Hivyo ni dhahiri kwamba wazazi hao wenyewe ni kielelezo bora kwa wanajamii kwani wamewajibika katika kuwaelekeza wana wao kupitia tenzi hizi. Ni wajibu wa vijana wao kuyafuata mawaidha waliopewa ili kuwaongoza maishani mwao bila hivyo watajuta. Aidha katika utenzi wa *Siraji* kwenye Kijumwa anamshauri Helewa kwamba ni wajibu wake aulize nasaha kutoka kwa rafiki na afuate yale mazuri. Anasema haya:

> "Rafiki wako wa kheri,
> Akupendao mkiri,
> Hoyo mtake shauri,
> Uyandame yenye ndia." ub. 65.

Katika ubeti 205, Kijumwa anamshauri Helewa kwamba ili kupata baraka kutoka kwa Mungu ni sharti awajibike kufuata mawaidha amepewa ili yawe kama dira ya kumwongoza kwenye safari yake maishani. Vile tulisema hapo mwanzo ni kwamba utenzi *Siraji* umepewa jina siraji kwa maana ya taa ili kumwongoza Helewa na wanajamii wengine kuishi kwa maadili yanayohitajika katika jamii. Hivyo lengo la Kijumwa ni kuwaona wanajamii wakiishi kwa njia ya kiadilifu ndiposa akautunga utenzi huu ili ujumbe huu upitishwe kutoka kizazi kimoja hadi kingine hata wajukuu watakaozaliwa baadaye ikiwa amefariki waupate ujumbe huo pia. Tazama beti hizi:

> “Chuo hiki ina lake,
> Ni siraji uishike,
> Kwa wanaume na wake,
> Wape wakitembea.” ub. 4.
>
> “Mushike wasia wangu,
> Nimezowambia wanangu,
> Tawabariki Mungu,
> Hini dira safiria.” ub. 205.

Vilevile, Kijumwa na Robert wote wametoa ushauri sawa kuhusu wajibu wa wana wao wa kiume kwa wake wao. Wamewashauri kuwapenda wake wao pamoja na watoto na kuwajibika kwa kuwatimizia mahitaji yao ya kimsingi. Aidha wamewakumbusha kwamba wana wajibu wa kuwaheshimu na kuwatii wazazi ili kupata baraka. Katika utenzi wa *Siraji* Kijumwa anasema haya kuhusu wajibu wa Helewa kwa mke wake:

> “Mke wako mpumbaze,
> Kwa uwezalo mweneze,
> Na wewe simteleze
> Nde ukalimatia.” Ub. 171.

Ujumbe zaidi kuhusu wajibu wa Helewa kwa wazazi, mke na watoto uko katika ubeti 84 na118 ambapo mtunzi anamhimiza Helewa kutii wazazi na asiwahi kuwakemea kwa sababu yoyote ile ama kuwatolea maneno ya kuwaudhi kwani katika utenzi wa *Adili* ubeti 59 Robert sawia na Kijumwa anamshauri mwanaye kwamba atakapopata jiko ampende mke wake na asimkosee ila tu mke amuanze yeye. Amesema haya kuhusu wajibu wa Adili kwa mke wake:

“Sita ukioa mke,
Kwa mapenzi mshike,
Simfanyie makeke,
Ila akuanze yeye.”ub. 59

Beti zingine zinazoshughulikia zaidi kuhusu wajibu wa Adili kwa mke na watoto ni ubeti wa 62, 63 na 64. Ambapo anamshauri Adili kumheshimu mke ambaye ni mama ya watoto wake kwani kulingana na mafunzo ya dini ni sharti mama aheshimiwe kwa kazi ngumu anayoifanya ya kulea watoto. Aidha Adili ameambiwa kuwajibika kuwapenda watoto kadri ya uwezo wake na kuwapa mawaidha yatakayowasaidia kwa maisha ya baadaye.

**3.1.6 Umakinifu**

Kwa maoni yetu kuwa makini ni hali ya kufanya jambo kwa utulivu na kuwa mwangalifu katika kila jambo mtu atendalo au anenapo. Tunafahamu vyema ya kwamba kila jambo anenalo mtu au alitendalo lina matokeo yake ambayo yataweza kuwa mazuri au mabaya kutegemea na kitendo chenyewe. Mawaidha haya yamefasiriwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, ‘binadanu ni kiumbe aliye na wajibu wa kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.’ Hivyo basi mwanadamu akiwa mwangalifu katika matendo yake atajitenga na maovu ya kuwaudhi wenzake ili kujenga uhusiano mwema na kujiepusha na mizozo ya kila aina. Kwa kufanya hivyo itachangia kuleta utangamano miongoni mwa watu kisha kujiendeleza na kuishi duniani kwa furaha. Katika tenzi za *Siraji* na *Adili* watunzi wamewaonya wana wao kuwa waangalifu kwa kila jambo wanenalo au watendalo.

Kwanza kabisa kuwa na ulimi mzuri ni mojawapo ya maadili ambayo watunzi Kijumwa na Robert wameshughulikia kwa njia iliyo sawa. Vile tunaelewa ni wazi kwamba matamshi mabaya huweza kusababisha chuki na hatimaye kuleta vita katika jamii. Hivyo basi, ni jukumu la kila mtu kufikiri kabla ya kuyatoa maneno mdomoni na pia watu wazima ni sharti wawafunze wana wao kuwa makini kabla ya kutoa neno lolote mdomoni. Tunawaunga mkono watunzi Kijumwa na Robert kwa mawaidha dhidi ya matamshi kwani matamshi mara mingi yameleta tashwishi miongoni mwa watu hasa husababisha mzozo wa kikabila nchini ndiposa hivi maajuzi tukashuhudia wanasiasa kutiwa kizuizini kwa sababu ya matamshi ya chuki.

Mwanzo, Kijumwa anamshauri Helewa kuwa makini na kuchagua maneno kabla ya kuyatamka kwa sababu ulimi mbaya waweza kusababisha mzozo; pia anamshauri awe na makini kabla ya kufanya uamuzi wa jambo lolote. Haya yanathibitika katika *Kurani Takatifu* Inasema haya:

> "Huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu.
> Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu.
> Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui" sura ya (2: 216)

Tazama beti hizi:

> "Unenapo mkarami,
> Yateue ya usemi,
> Majaraha ya ulimi,
> Hupoi yakikuingia." ub. 67.

> "Kheri neno kuteua,
> La upanga litapoa,
> La ulimi hukuzua,
> Jaraha nimekwambia." ub. 68.

Isitoshe, Kijumwa anamshauri Helewa asiwe mwepesi kujibu jambo analoliambiwa kabla ya kulifikiria. Ni muhimu ajipe muda ndiposa aweze kujibu kwa umakinifu bila kubahatisha kwani huenda akajibu visivyo na kupoteza umuhimu wa jambo analoliambiwa kisha kujuta baadaye.

> "Mtu kikwambia neno,
> Sijibu upesi mno,
> Ingawa dakika tano,
> Kheri kwanda kusikia." ub.112.

> "Ukijibu kwa upesi,
> Nawe mwando huliisi,
> Utajibu ukaisi,
> Faida itakupotea." ub. 114.

Fauka ya hayo, Kijumwa katika ubeti 169 na 170 anamshauri Helewa awe mwangalifu anapochagua marafiki hasa mchumba awe kutoka familia yenye maadili na ni vyema awe kutoka jamaa yake ndiposa jina lake zuri lizidi kuwa maarufu. Haya mawaidha yanathibitika kwenye *Kurani Takatifu* sura ya 7:58 anamtahadharisha asijitie mtegoni kama panzi kwa kuwa na marafiki wenye mienendo hasi wasije wakamwingiza pabaya. Anasema haya:

"Usiyaweke matandi,
Baba angalia pandi,
Kwenda taani hatindi,
Hata akateketea." ub. 182.

Mtunzi Robert naye sawia na Kijumwa hakuchelewa kumwonya kijana wake Adili kujiepusha na matamshi yenye athari mbaya ambayo yangeweza kusababisha chuki katika jamii. Alimshauri ajifunze kusema bila kuwaudhi watu na ajihadhari kutumia lugha mbaya ambayo ingeweza kuleta hasara. Tazama beti hizi:

"Nne fanya taaluma,
Kujifunza kusema,
Neno linalochoma,
Bila udhuru usitoe." ub 40.

"Lugha mbaya hasara,
Inawakisha hasira,
Na kuleta madhara,
Hiyo yache pekee." ub. 44.

Aidha Robert anamwonya Adili kuwa mwangalifu asijiingize kwenye njia ambazo si adilifu ila aweze kufuata njia za nzuri ndiposa kufanikiwa maishani na kuishi kwa amani na raha. Anasema haya:

"Njia isiyo adili,
Iliyo na ukatili,
Hawendi makubeli,
Nawe usisafirie." ub. 83.

### 3.1.7 Heshima na adabu

Katika utafiti wetu neno heshima tumelichukulia kuwa ishara ya kuthamini. Ni hali ya kufanya adabu kwa Mungu au binadamu wengine. Watunzi Kijumwa na Robert wote wanawasisitizia wana wao kuwa na heshima kwanza kwa Mungu, wazazi, watu wazima, wakuu kazini, masikini na wenzao wa kiwango sawa. Ushauri huu ni wa muhimu sana kwani kwa kuzingatia heshima na adabu kutadumisha amani na kujiepusha na ugomvi pamoja na migogoro mengineyo katika jamii. Maoni hayo yanaongozwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa, 'mwanadamu ana wajibu wa kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahari pa kufurahia' Katika utenzi wa *Siraji* anayasema haya:

> "Na mkuu mtukuze,
> Na mtoto simtweze,
> Kwa maneno wapumbaze,
> Usifu na kuwetea*."* ub. 40.

Kijumwa anamshauri Helewa kuwa na heshima hata kwa walioshushwa madaraka na asiwacheke ila azidi kuwapa heshima ya awali. Mara nyingi watu huwakosea heshima walioshushwa mamlakani na hata kuwacheka. Aidha mtunzi anamwonya mwanaye dhidi ya kumdharau kilema kwani hata yeye ataweza jaaliwa ulemavu kwa njia moja au nyingine. Hiyo tabia sio nzuri ndiposa Kijumwa anaikemea kwa hali ya juu. Anasema haya:

> "Ukimwona terema
> Fanya za kwanza hishima,
> Wala siteke kiyema,
> Mara mngu hukukwetea*."* ub.43.

Robert naye anamshauri Adili kumheshimu Mungu ambaye anatambua kila jambo linalotokea na mwenye uwezo wa kuwapa waja wake mazuri ya kila aina. Mawaidha ya Robert kuhusu Mungu ameyafungamanisha na yale mafunzo ya dini kwenye *Kurani* katika sura ya 31:11
"Vyote hivi ameviumba mwenyezi Mungu. …" Inasema kuwa Mungu ndiye ameviumba vyote ulimwenguni mwanadamu akiwemo. Hivyo basi ni sharti aheshimiwe.

Aidha amemshauri kuwa na adabu kwa watu tofautitofauti kama viongozi na wazazi kila wakati ndiposa aweze kufanikiwa maishani. Vilevile, anamkumbusha umuhimu wa kuwa na adabu kwa wazazi, viongozi na watu wote kwa jumla bila kubagua. Ni wazi kwamba kwake Robert sawia na Kijumwa adabu na heshima ni mojawapo ya maadili muhimu sana na ni sharti kila mwana kuwa nayo. Ni dhahiri ya kwamba mawaidha haya ya Robert pia yanathibitika kwenye *Kurani Takatifu* katika sura ya 31:14-15.

"Na tumemuusia mwanadamu kuwafanyia ihsani wazazi wake mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu ..na wazazi wako wakikushurutisha kunishirikisha na yale ambayo huna elimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani  maadamu ni wazee wako …"

Hivyo basi ni sharti mwana kuwaheshimu wazazi na kuwashukuru kwa kazi ngumu waliofanya kuwalea tangu utotoni hadi utu uzima. Tazama beti hizi:

"Ajua yote kwa ghibu,
Bila kusoma kitu,
Ni bwana wa thawabu,
Wajibu aheshimiwe." ub. 19.

"Pili tii mfalme,
Wa kike na wa kiume,
Bila ya kinyume,
Utii uwatendee." ub 34.

Mawaidha mengine kuhusu heshima na adabu yanapatikana katika ubeti wa 34 na 36 kwenye utenzi wa Adili pale ambapo Robert anamsisitizia mwanaye kwamba ni jambo la busara kuyafuata yale aambiwayo na viongozi bila kuwabagua kijinsia ila awe mtiifu kwao. Aidha amemwambia kuhusu kuwaheshimu wazazi na kuwafanyia mazuri kwao kadri ya uwezo wake kwani kulingana na amri za Mungu; ni wajibu wa kila mwana kufanya hivyo ndiposa aweze kupata thawabu na hatimaye kuingia peponi. Hivyo basi ni dhahiri ya kwamba mawaidha ya watunzi hawa yana uhusiano wa karibu sana na yamefungamanishwa na dini ndiposa tukirejelea *Kurani Takatifu* katika sura ya 17: 23 inasema ya kwamba wazazi waheshimiwa na wana wao, na wana wasiwakemee ila waseme nao kwa msemo wa heshima.

Katika ubeti wa 46 Robert anamshauri Adili kwamba popote atakapokuwa aambatane na adabu ndipo ataona mazao mazuri. Hivyo tumeweza kuona ya kwamba Robert analipa kipaumbele swala hili la adabu. Anasema haya:

"Ambatana na adabu,
Uwe nayo karibu,
Ina mazao ajabu,
Shika usiache." ub.46.

**3.1.8 Utu wema na matendo mazuri**

Kama tulivyosema awali ni kwamba mtu anapotenda mambo mema anasemekana kuwa na utu. Matendo mema huleta sifa njema kwa sababu mambo mema ndio yanakubalika katika kila jamii. Mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuyachambua mawaidha haya ni ule unaobaini kuwa 'Fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii.' Watunzi Kijumwa na Robert katika utunzi wao wa tenzi za *Siraji* na *Adili* wanawiana kwa jinsi wamelishughulikia swala hili la utu. Kupitia matendo hayo mazuri jamii nzima itafaidika kwa kuishi kwa amani na kujiendeleza kimaisha kutokana na utangamano.

Kijumwa anamshauri mwanaye Helewa kuwa mwenye utu kama nyanyake kwa jina Kamari alivyotenda akiwa hai. Aliyafafanua matendo mema yakiwemo yale ya kuwasaidia wagonjwa hata wale wenye vidonda na harufu bila kuwadharau na kuwapa msaada wasiobahatika katika jamii kama masikini na walemavu, kufariji rafiki kwa msiba, akubali kutumwa na rafiki, kumsaidia rafiki yake anapopigwa, kutoa mkopo kwa wanaohitaji, kusaidia kutatua mzozo kati ya wawili wanaopigana bila kupendelea miongoni mwa matendo mengi mazuri Kijumwa aliyoyataja.

Kijumwa anamshauri Helewa ya kwamba masikini akija kwake kuomba ni heri ajikakamua na kumpa angalau vichache ndiposa atabarikiwa. Pia amemshauri Helewa ya kwamba awe mwepesi kumfariji rafiki yake aliyepata msiba kuliko vile anavyomtembelea akiwa na sherehe. Matendo hayo mema nimeyataja hapo juu yako kwenye beti hizi 15, 19, 20, 23, 29, 31, 39, 52, 71. Tazama beti hizi:

"Na uchenenda ndiani,
Ukiona masikini
Ulo nacho mfukoni,
Mpe naye ngaa moya." ub 71

"Kwa mamangu walikiya,
Magonjwa yamewaneya,
Sikuona siku moya,
Pua akiwashikia." ub. 75.

Robert naye sawia na Kijumwa, katika utunzi wake anasisitiza utu kuwa jambo la muhimu maishani. Katika kazi zake nyingi amesawiri wahuka wenye utu wakifanikiwa maishani hasa ile kazi ya *Utubora Mkulima*. Katika tawasifu yake *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini* anatueleza jinsi yeye mwenyewe alikuwa na utu hata kazini ndiposa akafanikiwa kupandishwa vyeo. Aidha katika utenzi wa *Hati* anamtahadharisha binti yake kujitenga na kutu yaani matendo maovu yatakayomletea aibu. Katika utenzi wa *Adili* ubeti wa 81, 82 na 85, Robert anamshawishi Adili awe mkarimu na aweze kutoa msaada awezao. Pia anamwonya kwamba akijitakia makuu huku wengine wasipate hakuna heri hivyo basi ni vizuri kuwajali wenzake. Tazama beti hizi:

"Msaada ukiweza,
Kutoa ni mwangaza,
Ambao utatukuza
Jinalo lisipotee." ub. 81.

"Kutaka yote wewe,
Wengine wasipewe,
Hakuna heri mwishowe,
Hilo usikusudie." ub. 82

**3.1.9 Kuweka siri**

Watunzi Kijumwa na Robert wote wameshughulikia umuhimu wa kuweka siri. Ni Jambo la kawaida kwamba mtu hapaswi kufichua siri yake ovyo ila tu kwa wachache wapasao kujua ndiposa mtunzi Kijumwa anamtahadharisha Helewa kwamba asifunue siri yake hasa kwa adui isipokuwa yule tu anayemwamini. Anasema haya:

“Sifunuwe siri yako,
Khasa kwa adui yako,
Na kwa yeyote ni miko,
Ila mezokusafia” ub. 203

Robert naye sawia na Kijumwa anamwonya mwanaye Adili dhidi ya kutoa siri zake ovyo kwa watu asiowamini. Anasema haya:

“Hadhari usiache,
Siri yako ifiche,
Ila watu wachache,
Wapasao wajue.” ub. 77

Hivyo tunapata kwamba hizo beti mbili zinaingiliana sana kama kwamba ni mtunzi mmoja ameyatoa mawaidha hayo. Ni dhahiri kwamba watunzi Kijumwa na Robert wote wanapendelea vijana wao kuweka siri ili kufanikiwa maishani.

### 3.1.10 Malezi bora

Malezi ni jinsi ya kumkuza mwana kulingana na taratibu zilizokubalika. Aidha tunaweza kusema ya kwamba malezi ni njia ya kukuza watoto kwa kuwafundisha tabia au maadili yanayostahili. Kama tulivyosema hapo mwanzo malezi huanzia kwenye familia, kabla ya watoto kupelekwa shuleni. Mzazi ana wajibu muhimu wa kumkuza mwanaye. Watunzi Kijumwa na Robert ni kielelezo muhimu katika jamii zao mahususi kwani tunawaona wakiwaelekeza wana wao jinsi ya kuishi. Ushauri huu unaambatana na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, ‘fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii.’ Imedhihirika wazi kwamba, Kijumwa na Robert kupitia utunzi wao wamewapa wana wao mawaidha, licha ya wana hao kuwakosa wazazi wao wa kike kwani Adili alikuwa amefiwa na mama huku Helewa alimkosa mama yake karibu kwa kuwa walikuwa wametengana na baba.

Hata hivyo, tunaona kwamba Helewa na Adili wangefanikiwa maishani kwa kuyazingatia mawaidha waliyopewa na wazazi wao. Hivyo ni dhahiri kwamba jukumu la kulea wana ni la wazazi wote na ikiwa mzazi mmoja hayuko kwa sababu zisizoepukika haimaanishi kwamba

mwana atayakosa malezi. Watunzi Kijumwa na Robert wamewaelekeza wana wao Helewa na Adili jinsi ya kuwalea wana wao watakapokuwa wazazi. Licha ya Kijumwa kumshawishi Helewa katika ubeti 47 kutowaacha wana wake wa chuoni kuombaomba majumbani, pia amemwonya kutumia lugha chafu mbele ya watoto na asiwape watoto wake fursa ya kutukana na kupiga watu kwani watazoea tabia hiyo hasi. Tazama beti hizi:

> "Simshauze kijana,
> Ziumbe wakikutana,
> Kipija kiwatukana,
> Kabisa simpe ndia." ub. 111.

Mtunzi Kijumwa pia amemshauri Helewa ya kwamba ni muhimu kumfunza mwanaye kumcha Mungu. Hivyo basi ni jukumu lake Helewa kama vile alivyofanya babake kutomwaacha amwaasi Mungu; naye aweze kumwelekeza mwanaye kwa njia zinazostahili na kumrekebisha kila wakati anapotenda maovu. Tazama ubeti huu:

> "Na mwano kumuawini
> Kwa kuasi Rahamani,
> Sitilie shirikani,
> Sandame hapana ndia." ub. 118.

Robert naye sawia na Kijumwa amemshauri Adili kuwalea wanawe kwa kuwafunza kila namna ya adili kabla ya kuwapa mali. Tunamuunga mkono mtunzi kwa hayo mawaidha kwani ni kweli tumeshuhudia watoto wengi ambao wanarithishwa mali bila kufunzwa maadili na baadaye wanatumia mali hayo vibaya na kuangamia. Hivyo basi ni sharti kila mwana apate maadili kabla ya kurithishwa chochote na kwa kufanya hivyo atajua kulinda hayo mali. Anamsisitizia kuwapa wana funzo la nguvu ili kuamsha akili yao; afanye jitihada kuwapa mawaidha na kuwasisitizia kuyafuata ili kuishi vyema kwani bila kufanya hivyo atakuja kujuta kwa mtoto wake kupotea. Mawaidha hayo yamefasiriwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, 'Fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii.' Kupitia malezi mema ya watoto jamii nzima hufaidika kwa vile watoto watakuwa na msingi thabiti wa kujiendeleza maishani. Anasema haya katika beti hizi:

“Wafunze taamli,
Kila namna adili,
Kabla kuwapa mali,
Watoto watumie.” ub. 64.

“Hazina na ulegevu,
Kwa mtoto upotevu,
Mpe funzo la nguvu,
Kuamsha akiliye.” ub. 65.

**3.1.11 Ushirikiano na uhusiano mwema**

Ushirikiano ni hali ya watu kuungana na kusaidiana katika shughuli. Ili watu kushirikiana ni sharti kuwe na uhusiano mwema na uelewano kati ya wanaohusika. Watunzi Kijumwa na Robert wote wanasisitiza umuhimu wa uhusiano mwema na ushirikiano katika kila jambo. Kijumwa katika ubeti wa 18 anamshauri Helewa kufanya urafiki wa kheri na wengine ili kuulizana ushauri. Aidha ubeti 19 anamshauri kuwapatanisha wanaozozana ili kujenga uhusiano mwema na maelewano kati ya wanajamii.

“Fanya swahibu wa kheri,
Kwa kutakana shauri,
Ugawadi tusikiri,
Swahibu akitwambia.” ub. 18..

“Na mwendo ukimkuta,
Yeye na mtu huteta,
Siwapendelee zita,
Amua uchangukia.” ub. 19.

Aidha Kijumwa anamshauri Helewa kushirikiana na kushauriana na wenzake hata kama akiwa ugenini. Hivyo basi anaonyesha dhahiri kwamba mtu hawezi kufanikiwa peke yake ni sharti aungane na kusaidiana na wenzake. Anasema haya:

“Ukiwako ugenini,
Ukamuona mwendani,
Wa ishifaki amini,
Shauri na liwe moya.” ub. 117.

Robert naye sawia na Kijumwa anamshauri Adili kufanya urafiki na walio karibu naye na kuwapenda watu wote ili kujenga uhusiano na jina lake pia kutupilia mbali upweke kwani unachukiza. Aidha amemshauri Adili kupendana na watu wote hata aliye mbali na afanye juhudi kusikilizana na walio karibu na awe kipenzi mpaka wengine watamani awe rafiki yao. Hayo yote ni thibitisho tosha kwamba kwake Shaaban uhusiano na ushirikiano ni jambo la muhimu sana katika jamii. Robert anasema haya:

> "Patana na masahibu,
> Ulio nao karibu,
> Kwao uwe muhibu,
> Wa mbali wakuanie." ub. 68.
>
> "Huyu kumpenda yule,
> Ni asili ya umbile,
> Upeke jambo tule,
> Huchukiza uvundoye." ub 69.

**3.1.12 Msamaha**

Msamaha ni tendo la kuomba radhi kwa mtu aliyekosewa. Msamaha ni jambo la hekima kwani laweza kutatua mzozo ambao ungesababisha maovu kama vile vita. Hivyo ni muhimu kuomba radhi kwa Mungu na kwa binadamu wenzetu ili kuendeleza uhusiano mwema. Watunzi Kijumwa na Robert wamewiana kwa jinsi wamelishughulikia swala hili la kuomba msamaha. Kupitia mhimili wa nadharia iliyotuongoza kuwa 'fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii,' watunzi wametekeleza wajibu wao kwa kuwafafanulia wanajamii umuhimu wa kuomba msamaha ikiwa mtu amekosea ili kuregesha uhusiano mwema na wenzake. Hivyo basi kupitia tenzi hizi funzo muhimu hujitokeza ya kwamba msamaha ni njia mwafaka ya kutatua matatizo katika jamii.

Katika utenzi wa *Siraji* swala la msamaha linajitokeza katika ubeti 70 na 189; Kijumwa anamshauri Helewa kwamba siku zote akifanya makosa atubu kwa Mungu na atapata msamaha. Aidha, katika ubeti wa 189 Kijumwa anamshauri Helewa ya kwamba mke anapomtoroka na akirudi mwenyewe awe na subira amsamehe na kumkubali kwa sababu atakuwa amepata adabu. Mawaidha haya ya msamaha pia yanathibitika kwenye *Kurani* katika sura ya (49:12) "…*bila shaka Mwenyezi Mungu ni ni mwenye hupokea toba na mwingi wa kurehemu*." Tazama ubeti huu

“Kurani hutwambia,
Nawe soma hiyo aya,
Toba ukitubia,
Toba Mngu hupokea.” ub.70

Katika utenzi wa *Adili* pia Robert amelishughulikia swala la msamaha katika ubeti wa 60 na 61. Amefafanua umuhimu wa kuomba msamaha ya kwamba huleta furaha kwa anayepokea na kwa anayetoa. Anaendelea kusema ya kwamba kwa kuomba msamaha atapata suluhisho ya mambo maovu ambayo yangeleta hasara kutokana na chuki hivyo basi kuleta amani na furaha kwa waliozozana.Tazama ubeti huu:

“Hata hivyo ukiweza,
Samahani kufanyiza,
Faida itafuliza,
Kiwajia yeye na nawe.” ub. 60.

Mtunzi Robert sawia na Kijumwa pia anamshauri Adili kumwomba Mungu msamaha wa dhambi na Mungu atamsamehe kwani hakuna mwanadamu aliye mkamilifu. Kwake Mungu viumbe vyote ni dhaifu hivyo ni kawaida mwanadamu kutenda maovu basi ni vyema kuomba msamaha na Mungu atamkubali anayetubu. Anasema haya:

“Mwombe daima Rabi,
Akusamehe madhambi,
Mwanadamu ni vumbi,
Makosa desturiye.” ub. 26.

**3.1.13 Kuwa na upole**

Watunzi Mohamed Kijumwa na Shaaban Robert wamewasisitizia vijana kuwa na upole na wasiwe wanajiona kwa sababu yoyote ile. Kijumwa anasema ya kwamba hakuna haja ya mtu kujisifu kwa jambo lolote lile kwani yote hutendeka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi anasema kwamba si jambo la busara kwa mwanadamu kusema ya kwamba ni yeye pekee kwani Mungu tu ndiye halinganishwi na kiumbe chochote basi bila shaka sifa zote zimwendee Yeye. Tazama ubeti huu:

“Usiiyone mwenyewe,
Kama hakuna kamawe,
Ujuba na upunguwe,
Na kiburi kuitia.” ub. 89.

Katika ubeti wa 183 Kijumwa anamtahadharisha Helewa dhidi ya kujisifu. Anamwonya kwamba kujipigia debe kunaweza leta mambo mabaya kwa maisha yake. Hivyo basi ni heri anyenyekee kwa Mungu na Mungu atamuinua. Anasema haya:

“Ukipendwa mtu wewe,
Fahamu siishauwe,
Kuisahau mwishowe,
Maovu hukudhulia.” ub 183.

Katika ubeti wa 87 Robert naye sawia na Kijumwa anamwonya Adili dhidi ya kujiona kuwa bora zaidi ya wengine. Anamwambia ya kwamba mtu hajipi sifa ila apewe. Hivyo ni dhahiri kwamba watunzi Kijumwa na Robert hawaoni haja ya mtu kujisifu badala yake mtu anastahili kutoa shukrani kwa Mungu ambaye hutoa yote.

“Ukidai kuwa bora,
Jua watiwa fora,
Hajipi sifa bora,
Mtu ila apewe.’’ ub. 87.

Katika kuhitimisha kazi zao tunaona watunzi Kijumwa na Robert wameweka wazi asili zao. Hili ni thibitisho tosha kwamba watunzi wenyewe hawaoni haja ya kujidai. Kijumwa katika ubeti wa mwisho 209 anamwambia Helewa kutilia maanani ushauri aliyompa yeye fundi Kijuma bin Bwana Ikirama Al-Bakari asili. Robert naye sawia na Kijumwa ameweka wazi asili yake katika ubeti wa 97-100. Ameelezea kwamba yeye ni mwafrika si mwaarabu, mhindi wala mzungu. Hii inaonyesha ya kwamba watunzi hawa hawajitakii makuu kwani wanakubali asili yao.

Utenzi wa *Adili* tunayapata haya:

“ Msidhani mahuluti,
Kabila sikusaliti,
Mwafrika madhubuti,
Vingine nisidhaniwe.” ub. 98.

“Si mwarabu si mzungu,
Hindi si jadi yangu,
Naarifu walimwengu,
Wadadisio wajue.’ ub. 100.

**3.1.14 Uvumilivu**

Uvumilivu ni hali ya kuwa na moyo wa kustahimili mambo magumu hasa wakati wa huzuni. Hali hii inasaidia sana kwani tujuavyo mvumilivu hula mbivu. Hivyo basi ni sharti mwanadamu ajue ya kwamba katika maishani kuna wakati wa furaha na wakati wa huzuni na ajitayarishe kukabiliana na changamoto ulimwenguni bila kujitia mashaka. Mawaidha haya yanatiwa nguvu na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, ‘mwanadamu ana wajibu wa kutekeleza ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.’ Hivyo basi licha ya changamoto azipitiazo mwanadamu ulimwenguni anastahili kutafuta njia mwafaka za kuepukana nazo ili kuendelea na maisha yake kawaida.

Katika ubeti wa 97 Kijumwa anamshauri Helewa ya kwamba awe mstahimilivu ikiwa amezingirwa na shida na hana fedha na asipandwe na mori. Mtunzi anamwonya mwanaye dhidi ya kuwa na hasira kwa sababu anajua kwamba hasira humwelekeza mtu kufanya maovu kisha kujuta baadaye. Hivyo ni muhimu kujitahidi kustahimili katika kila jambo ili kuepukana na ghadhabu ambayo huleta hasara. Amesema haya:

“Mambo yakikuzingia,
Nyumbani huna rupia,
Wata hasira kungia,
Na zitunu kuzitia.” ub. 97.

Robert naye katika utenzi wa *Adili* anamshauri Adili kwamba akipandwa na mori ni jambo la busara ajifanye kama bubu yaani asinene kwa sababu atakayoyatamka pengine yanawezaleta madhara makubwa na kusababisha mzozo kati yake na wenzake. Hivyo anamshauri kwamba ni heri atulize hasira yake kabla ya kutamka jambo lolote.Tazama:

“Ukiwa na ghadhabu,
Jifanye kama bubu,

Kimya ni utibabu,
Wa hasira uelewa." ub 47.

Kwa ufupi tumeweza kupata ya kwamba mengi ya maadili ambayo watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia katika tenzi zao *Siraji* na *Adili* yamewiana sana. Watunzi hao wameonyesha umuhimu wa watu kuzingatia maadili ya aina mbalimbali kwani wasipofanya hivyo huhatarisha maisha yao kutokana na migogoro itakayozuka kisha kukosa amani. Mawaidha hayo wameyatoa watunzi yamefasiriwa na mhimili muhimu wa nadharia ya maadili iliyotuongoza kuwa 'fasihi ina wajibu wa kutekeleza katika jamii.' Hivyo basi, tumeendelea na kubaini sababu za kuwiana kwa watunzi hawa katika kijisehemu kinachofuata.

### 3.2 Sababu za kuwiana kwa watunzi Kijumwa na Robert kwa jinsi wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume

Sababu kubwa ya kuwiana kwa watunzi hawa Kijumwa na Robert ni kwamba watunzi hawa ni waumini wa dini moja ya Kiislamu. Hivyo basi, mawaidha ambayo walioyatoa yamefungamanishwa na mafunzo ya dini ndiposa wamerejelea *Kurani* kitabu takatifu cha waumini wa dini ya Kiislamu kila mara wanaposisitiza maadili hayo. Hivyo basi maingiliano ya karibu miongoni mwa tenzi hizi *Siraji* na *Adili* yamesababishwa na dini. Mawaidha walioyatoa watunzi Kijumwa na Robert yanaoana na maoni ya wafuasi wa nadharia ya maadili iliyotuongoza katika utafiti wetu hasa Plato na Tolstoy kuwa 'fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii na maadili ni muhimu yajikite katika dini.' Tumebaini ya kwamba tenzi za *Siraji* na *Adili* zinasisitiza tabia chanya na beti zao nyingi zimefungamana na mafunzo ya dini.

Watunzi Kijumwa na Robert wanapotoa ushauri wao mwanzo kabisa wamewashauri wana wao kumcha Mungu. Hivyo kuonyesha ya kwamba binadamu akimcha Mungu mwanzo na mengine pia yatakuwa rahisi. Vile tujuavyo kiini cha dini ni kumfanya binadamu aishi maisha yenye maadili kwa kutarajia kupata malipo baada ya kifo. Watunzi Kijumwa na Robert wanaamini kuwepo kwa maisha baada ya kifo ndiposa wanasisitizia wana wao kuwa na maadili yanayohitajika katika familia na jamii kwa jumla ili kuelewana na wenzao wanapotangamana na kuishi kwa amani ndiposa baada ya kifo wapate kuingia peponi.

Kwa kuwashauri wana wao tunaona watunzi Kijumwa na Robert mwanzo kabisa wanatoa ushauri wa wana kumcha Mungu. Hii ni kwa sababu wanaelewa ya kwamba mtu yeyote akimwamini Mungu katika kila jambo ni sharti azifuate sheria za Mungu ambazo humwelekeza mtu kutenda mema kila wakati. Hivyo basi kwa kumcha Mungu maadili yote yatajitokeza katika maisha ya mtu bila kutarajia.

### 3.3 Hitimisho

Katika sura ya tatu, tumejadili jinsi watunzi Kijumwa na Robert wamewiana katika kushughulikia maadili ya vijana wa kiume kwenye tenzi zao *Siraji* na *Adili*. Maadili yanayowiana katika tenzi hizi ni: dini na imani kwa Mungu, elimu, ndoa na mapenzi, bidii kazini, uwajibikaji, umakinifu, heshima na adabu, utu wema na matendo mazuri, kuweka siri, malezi bora, ushirikiano na uhusiano mwema, hasira, msamaha na kuwa na upole. Hatimaye tumebaini sababu za kuwiana kwa watunzi hao. Sura inayofuatia ya nne tumeshughulikia kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert katika jinsi wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume.

## SURA YA NNE

## JINSI WATUNZI WA TENZI *SIRAJI* NA *ADILI* WANAVYOTOFAUTIANA NA SABABU ZA KUTOFAUTIANA KWAO

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii ya nne tumechambua jinsi ambavyo watunzi Kijumwa na Robert wanavyotofautiana katika kushughulikia maadili ya vijana wa kiume katika tenzi zao *Siraji* na *Adili* na sababu za kutofautiana kwao. Hivyo basi tumeweza kutambua kwamba licha ya watunzi hawa kuwiana sana katika kazi zao, pia wametofautiana kwa kiwango kikubwa. Mtunzi Kijumwa tofauti na Robert ameyashughulikia maadili mbalimbali tofauti na yale aliyoshughulikia Robert. Maadili hayo ni pamoja na: subira, haki na upatanisho, kufariji, dharau, tamaa ya vitu vya watu, tabia za maakuli, ubishi, kusengenya, kutojisifu, kutowapiga wanyama, kutania, kushtaki, kujipendekeza, usaidizi, talaka, udaku miongoni mwa mengineyo.

Robert naye, ameyashughulikia maadili tofauti na yale ambayo Kijumwa ameyashughulikia. Maadili hayo ni pamoja na: ahadi, chuki, uhusiano na masahibu, ubinafsi na mengineyo. Aidha kuna maadili ambayo yameshughulikiwa katika utenzi wa *Siraji* na wa *Adili* lakini watunzi wametofautiana kwa jinsi wameyashughulikia maadili hayo. Mfano wa hayo maadili ni: swala la ndoa. Maoni ya Kijumwa kuhusu ndoa hutofautiana na yale ya Robert kwa sababu licha ya Kijumwa kushughulikia swala la ndoa, pia ametoa maoni yake kuhusu talaka, naye Robert sawia na Kijumwa ameshughulikia ndoa lakini hakutoa maoni yake kuhusu talaka. Hivyo basi tumeanza kwa kuchunguza maadili ambayo Kijumwa ameyashughulikia katika utenzi wa *Siraji* na yanatofautiana na yale ya Robert katika utenzi wa *Adili*, kisha baadaye tumeyachambua yale maadili katika utenzi wa *Adili* na hutofautiana na yale ya Utenzi wa *Siraji*.

### 4.1 Maadili katika utenzi wa *Siraji* yanayotofautina na ya utenzi wa *Adili*

Katika kijisehemu hiki tumeyashughulikia maadili ambayo yako katika utenzi wa *Siraji* tofauti na yale yaliyoko katika utenzi wa *Adili*.

### 4.1.1 Subira

Subira ni hali ya kuwa na uvumilivu. Mtu akipatikana na jambo baya anafaa kuwa na subira kwani subira huvuta heri. Katika utenzi wa *Siraji* swala la subira linajitokeza katika beti za 49, 50, 56, 58, 59, 83 na 159. Katika ubeti wa 49 na 50 Kijumwa anamshauri Helewa kuwa mvumilivu kwa wagonjwa akitoa mfano wa wale wameugua ugonjwa wa kifua kikuu aweze kuwahudumia bila kuchoka hata kama ugonjwa utachukua muda mrefu asilalamike ila Mungu atampa malipo. Aidha anamshauri kwamba hata kama ugonjwa uwe wa gharama na kusababisha upungufu wa pesa bado awe na subira ya kumuuguza wala asimfukuze mgonjwa nyumbani kwa kumkasirisha; akiwa mkali kwa kutotaka pengine kutumia dawa au kukataa kula ni heri amvumilie hadi pale atakapopona au kufa. Mawaidha hayo ya subira yanathibitika kwenye *Kurani* inasema:

"..Enyi mlioamini! Jisaidieni katika mambo yenu kuwa kwa subira na sala; bila ya shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri….Ambao uwapatao msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu.." sura ya 2: 153-157.

Tazama beti hizi:

"Simtoe mtu kwako,
Hata kiwa na ukoko,
Kakutia maudhiko,
Subiri akikwambia." ub 49.

"Muwee kikuwalia,
Siku zikaendelea,
Ukali kakufanyia,
Tukua moyale huya." ub. 50

Katika ubeti wa 58 na 59 Kijumwa anamshauri Helewa kwamba subira ina faida yake baadaye hivyo ni muhimu ajifunze kuwa nayo na asiwe mtu wa kulalamika ovyo kwani huenda akazikosa thawabu kutokana na malalamiko yake. Hivyo ni muhimu kuvumilia na kumwomba Mungu katika kila jambo hata kama shida zitakuwa nyingi; afungwe hata jela na hata kufa, Mungu atamlipa. Hivyo basi ni bora kuwa mvumilivu kwani mwishowe Mungu atampa nguvu za kushinda kila aina ya majaribu. Kijumwa anampa mawaidha ya kwamba akizidiwa na maumivu ya ugonjwa awe na subira na kumwomba Mungu amsaidie. Tazama beti hizi:

“Ukiwaa wewe mara,
Ukizidi mihayara,
Kheri kuwa na subira,
Ukimwomba Jaliya.” ub 56.

“Subiri subira njema,
Sidumu na kulalama,
Mwishowe huya malama,
Ukilalama si dawa.” ub. 58.

Katika ubeti wa 83 Kijumwa anamshauri Helewa kwamba akiandamana na mwenzake njiani asimwache ikiwa anazungumza na mwenzake. Ingawa atachoka si vyema kumuacha rafikiye.

“Na mwendo mukifuatana,
Kaya mtu wakanena,
Kungoja wachoka sana,
Si njema kumkimbia.” ub. 83.

Aidha katika ubeti wa 159 Kijumwa anamshawishi Helewa kwamba asibabaike kwa kuenda mbio sana kutafuta ila akumbuke Mola ndiye anatoa riziki. Hivyo basi amwachie Mungu mambo yote kwani yeye ndiye hutoa na kuchukua.Ni muhimu awe mvumilivu kwani mwishowe Mungu atambariki. Tazama ubeti huu:

“Wata na kupapatika,
Moliwa wako kumbuka,
Mola hupa na kupoka,
Subiri atakuletea.” Ub. 159.

**4. 1.2 Tabia za maakuli**

Kijumwa ametoa mawaidha mengi sana yanayohusiana na maakuli katika beti 128-166. Mtunzi anamshauri mwanaye kutojisifu kwa chakula alacho na pia akiwa karamuni asiwe na tamaa ya kula huku akiangalia sahani zingine zinazoletwa ila tu aridhike na kile chakula alichopewa. Ikiwa anazungumza na chakula kinaandaliwa hafai kuacha kuzungumza na kuangalia kile chakula. Kwake mtunzi Kijumwa haifai hiyo tabia kwani inaonyesha tamaa kwa kile chakula

kama kwamba atakuwa anadadisi ni sahani gani itatiwa chakula kingi ili kuichukua hiyo. Kijumwa anamshauri Helewa kutoangalia juu kwenye sahani zinazoletwa anapokula kwani hiyo huonyesha tama

Katika ubeti wa 134 Kijumwa anamwonya Helewa dhidi ya kufuta mkono wake ukingoni mwa sinia kama njia ya kuusafisha na pia anamshauri ya kwamba anapokula asitie mkono wote kinywani kwani tabia hizo zinaweza kuwaudhu wale wenzake na kuwakosesha hamu ya kuendelea kula. Aidha katika ubeti wa 135, mtunzi anamwonya Helewa dhidi ya kukivuta chakula kingi upande wake anapokula na wenzake kwenye sinia tabia; hiyo pia ni hasi na inaonyesha ubinafsi. Pia anamwonya kuchagua na kujivutia vipande vikubwa vya nyama na kuwakosesha wenzake kupata. Kwake Kijumwa hiyo ni tabia ya aibu sana. Kipande cha nyama kikianguka karibu na mwenzake ni vizuri akiachie mwenzake ili kujiepusha na aibu. Tazama beti hizi:

> “Na kufuta ukingoni,
> Kwa mkono sahanini,
> Zanda kutia kanwani,
> Hayo hushinda pia.” ub. 134.

> “Na kuteua zinofu,
> Ambao zilo nadhifu,
> Ili ruhu kuidhifu,
> Aibu hukuivutia.” ub. 135.

Vile vile, Helewa ameonywa kula haraka haraka kwani hiyo huonyesha tamaa ya kutaka kula chakula kingi kuliko wenzake ambapo ni hatari sana ikiwa chakula kitamsakama kooni. Hivyo Kijumwa anamshauri Helewa kula taratibu kwani ndio ustaarabu na pia ajenga sifa yake.
Kijumwa anamshauri kutoramba vidole anapokula na wenzake kwa sababu huenda akawaudhi kisha kuwapotezea hamu ya chakula hicho na kisha kumsengenya baadaye kutokana na tabia hizo. Tazama beti hizi:

> “Kula upesi upesi,
> Na hilo huinukusi,

Fanya mambo kwa kiasi,
Mara zitakupalia." ub. 137.

"Kuna lingine nda kwanda,
Kula ukiramba zanda,
Fahamu watu hutunda,
Watakwamba kisa pia." ub. 138.

Baada ya karamu Helewa anashawishiwa kuandamana pamoja na wenzake ili kuondoka kwa furaha akimsifu Mungu kwani ndiye aliyemjalia hayo yote. Vilevile kama chakula kimepikwa vizuri anastahili kuwasifu wapishi mbele ya umati lakini ikiwa chakula si kitamu asiseme wala asieneze habari hizo kwa sababu huenda akawaibisha waliokitayarisha. Akiwa ameshiba aondoke upesi bila kuchelewa lakini wenyewe wakimwomba kuketi kidogo ni heri afanye hivyo. Kwa maoni yetu tunaona kwamba kule kuondoka haraka kutasaidia Helewa asionekane kwamba anahitaji pengine chakula zaidi na pia atawapa wageni wengine fursa ya kukaribishwa. Kwa upande mwingine mtunzi anamshauri Helewa asubiri kidogo anapoulizwa na wenyewe ili asionekane kama kwamba haja yake ilikuwa ni chakula tu. Hayo yapo katika ubeti 139-142.

Katika ubeti 143-147, Kijumwa anampa Helewa mawaidha ya kwamba ikiwa hakualikwa kula chakula basi hafai kula bila ruhusa ya mwenyewe. Pia ikiwa ni sherehe hafai kuhudhuria bila mualiko wala kuomba kutiliwa chakula. Hayo mawaidha huthibitika kwenye *Kurani*. Tazama:

"..msiingie nyumba za Mtume ila mpewe ruhusa kwenda kula, pasipo kwenda kukaa kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa ingieni na mnapokwisha kula tawanyikeni." sura ya 33:53.

Hivyo basi ni dhahiri kwamba Kijumwa amefungamanisha maadili yake na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Anamshauri Helewa kutofautisha mualiko wa ukweli na usio. Hivyo basi, ikiwa anayemualika hajasisitiza basi kwa kutilia mkazo basi asikaribie. Tunamuunga mkono Kijumwa kwa hayo mawaidha kwani ni kweli kwamba watu wengi husema karibu ya mdomo kama desturi tu huku wakisubiri kuambiwa ahsante. Kwa hivyo ni sharti mtu asisitize ili kuonyesha mualiko wa kweli.

Kijumwa pia ameshauri ya kwamba mtu hafai kula huku akizungumza. Anamwonya Helewa kwamba chakula kikiwa mdomoni hafai kusema hadi akimeze mwanzo ili asije akawaonyesha wenzake chakula kilichotafunwa mdomoni na kuwakosesha hamu ya kuendelea kula. Aidha kwa kutoa mabaki mdomoni ni sharti afunge mdomo. Aidha anamshauri kwamba anapotumia kinywaji asinywe cha kuzidi wala kwa vishindo na kuvuta kwa kero. Hiyo tabia hasi huudhi sana. Tazama beti hizi:

"Na chai ikidhiri,
Usinwe kwa utiriri,
Kuvuta kwa kujihiri,
Au zumari kulia." ub. 153.

"Na kwa kiasi chako,
Usitupe ada yako,
Hasibu unwao kwako,
Na kwa watu ni mamoya." ub. 155

Kwake Kijumwa ni muhumu hata kama mtu amealikwa karamuni apike kwake na kula kama kawaida isiwe kama kwamba anategemea vile vyakula vya sherehe tu. Pia mtunzi amekashifu tabia za kuombaomba akitoa mfano wa kusumbua majirani kuomba mchuzi. Hivyo basi ni muhimu kula chakula ulichokipata kidogo kuliko kuwa na tamaa na kuhitaji zaidi ya uwezo wako. Tazama beti hizi:

"Uchambiwa karamuni,
Siwate mwako nyumbani,
Ukapunguza wizani,
Kheri kama mazoea." ub. 156

"Na ukipika azizi,
Wali hauna mtuzi,
Jirani usimuudhi,
Zikombe kumpekea." ub. 158.

Kwa ufupi ni mengi sana ambayo mtunzi Kijumwa ameyashughulikia kuhusu tabia za maakuli. Katika ubeti 160-166, ametoa mawaidha kuhusu usafi wakati wa kula kama vile kutokuwa na makamasi na kutema mate ovyo. Ni dhahiri kwamba tabia hizo huwaudhi wengine kisha kukosesha hamu ya chakula. Aidha, Helewa ameshauriwa kuwa na roho ya kusaidia pale anapoambiwa ya kwamba masikini pia ampe chakula kwa kumtilia sahani nzuri na pia akitaka kubeba apakuliwe. Tazama beti hizi:

> “Na akiya maskini,
> Hata kwenu karamuni,
> Simtilie wayani,
> Kheri sahani zengea.” ub. 161.

**4.1.3 Udaku na kusengenya**

Udaku ni hali ya kutafuta mambo ya watu kwa kutaka kuyajua na kuyaeneza kwa wengine ambao hata hayawahusu. Kusengenya pia ni hali ya kusema mtu kwa ubaya ikiwa hayupo. Kijumwa anamshauri Helewa kwamba kusengenya ni hatia na haikubaliki kwa Mungu kwani kwa kufanya hivyo yaweza kuleta matatizo. Aidha amemwonya dhidi ya kutaka kujua mambo ya watu kwa nia ya kuyaeneza kwa wengine ndiposa anamshauri kutojishughulisha na mambo ambayo hayamhusu. Anamshauri ya kwamba hata akijua mambo ya watu ni jambo la busara kuyanyamazia ili mambo hayo yasisambae na kusababisha mzozo. Katika ubeti wa tisa mtunzi amemwonya Helewa dhidi ya kuchunguza siri za watu ili kuzieneza. Kwake Kijumwa ni muhimu kuepukana na mambo ya watu ili kuepukana na mizozo. Mawaidha hayo yanathibitika kwenye *Kurani* sura ya 49:12 inasema:

“..wala msipeleleze habari za watu. Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine…”

Katika beti 100-102 Kijumwa anamshauri Helewa ya kwamba akiona mtu njiani amebeba kitu kwapani ama mfukoni kukiwa na kitu kimefungwa kwa karatasi asidadisi kujua ni nini ila huyo mtu mwenyewe amwelezee nini. Mawaidha hayo ni ya muhimu sana kwa sababu pengine mtu amebeba vitu vya siri na hataki kuuliziwa kuvihusu ataweza mujibu vibaya nakumwaibisha kisha kukasirika naye na kuanza vita. Tazama beti hizi:

“Na kumfatishi mwenyewe,
Mambo yake uyayue,
Na kunena kwa mayowe,
Apitao kasikia.” ub. 9

“Kusimama milangoni,
Kusikia walo ndani,
Uyayue hunenani,
Lepuke hatua mia.” ub. 104

### 4.1.4 Haki na upatanisho

Katika utafiti wetu, upatanisho tumeuchukulia kuwa hali ya kuwaleta watu au pande mbili zilizozozana kwa nia ya kuleta suluhu. Kwake Kijumwa ni muhimu sana watu wanapokosana waweze kutafuta suluhu kuliko kuchukiana na kupigana. Tunapata katika utenzi wa *Siraji* mtunzi anamshawishi Helewa kwamba akipata watu wakiteta asiwahimize kuendelea bali ni sharti afanye juhudi kuwapatanisha ili kuleta amani. Tujuavyo kuna watu ambao wana tabia hasi ya kushangilia watu wanapozozana badala ya kuwasaidia kutatua mizozo yao kisha baadaye kukatokea hatari ya vita na amani kukosekana. Ni jambo la busara kufanya juhudi kuleta amani katika jamii zetu na taifa kwa jumla. Hivyo basi Kijumwa kupitia utunzi wake alionelea kwamba ni muhimu kumpa funzo mwanaye kuhusu umuhimu wa amani. Anasema haya:

“Na mwendo ukimkuta,
Yeye na mtu huteta,
Siwapendelea zita,
Amua uchangukia.” ub. 19.

Aidha anamshauri ya kwamba mwenzake akipigwa asichelewe kuingilia kati ili kutafuta suluhu kwa kuwatenganisha bila kupendelea na kila mmoja amuonyeshe makosa yake kisha na kwa nia nzuri awalete pamoja. Hivyo ni dhahiri kwamba kwake Kijumwa katika kuwapatanisha wanaozozana ni sharti haki na ukweli kutekelezwa ili kuondoa wasiwasi miongoni mwa wanaopatanishwa. Tunamuunga mkono Kijumwa kwa mawaidha hayo kwani kwa kuwaleta wenzake pamoja kutazuia maovu katika jamii kama yale ya vita kutokana na fitina. Hivyo basi atachangia kuleta jamii pamoja kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Jamii yenye amani hujiendeleza kuliko ile yenye ugomvi. Tazama beti hizi:

“Na mmoya kwa mmoya,
Usiwe wa kwangalia,
Kati mwao kheri ngia,
Kwa haki ukiamua.” ub. 21.

“Sipendelee moyoni,
Fanya haki kwa mizani,
Usuluhishe wendani,
Kwako swafi yako nia.” ub.22

**4.1.5 Ushahidi**

Ushahidi kwetu tumeuchukulia kwa maana ya kutoa habari za kuthibitisha kwamba jambo fulani kweli lilitendeka au maelezo fulani ni ya ukweli. Mara nyingi kunapokuwa na tatizo la kutatuliwa kunahitajika mashahidi wa kuthibitisha waliyoyaona au kuyasikia yakiwa ya ukweli. Mashahidi wengine husema urongo ili kufanikisha lengo lao ndiposa tunaona Kijumwa anamuonya Helewa dhidi ya kutoa ushadidi wa urongo hata kama ni kwa kupewa pesa au kumtetea ndugu asikubali. Anamshauri kuelezea anayoyajua na kuepukana na asiyoyajua ili asilete utata katika kutafuta suluhisho la mzozo. Tazama beti hizi:

“Swahibu kupatikana,
Kenda kushtakiana,
Uyualo baba nena,
Usilijua kimbia.” ub. 26.

“Kuwa shahidi wa zuri,
Hata kwa nd uyo sikiri,
Kakupa fedha johari,
Ni kheri kutopokea” ub. 27.

**4.1.6 Kufariji**

Kufariji ni hali ya kumpa mtu moyo au kumliwaza aliye msibani ili aweze kuwa na matumaini na kuendelea na hali yake ya kawaida maishani. Kufariji ni njia moja ya kuonyesha kuwa mtu

anamjali mwenzake hasa katika shida ndiposa waswahili wakasema ya kwamba akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Mtunzi Kijumwa anamshauri Helewa kwamba rafikiye akipatwa na msiba afanye haraka kumfariji. Ni kawaida marafiki kuwakimbia wenzao wakipatwa na shida lakini kwake Kijumwa anaonelea ya kwamba rafiki wa kweli si yule ambaye anashirikiana na wenzake wakati wa furaha tu bali wakati wa shida pia. Tunamuunga mkono mtunzi kwa mawaidha hayo mazuri. Anasema haya:

"Bui wako msibani,
Upesi enda sikhini,
Zaidi ya karamuni,
Sikitika nawe ngia." ub 39.

**4.1.7 Tamaa ya vitu vya watu**

Kijumwa ameshughulikia sana swala la kuheshimu vitu vya watu. Mtunzi amemshauri Helewa ya kwamba akiwa kwenye nyumba za watu asiwe na tabia hasi ya kushikashika vitu bila ruhusa ya mwenyewe na kuulizia kuhusu hivyo vitu ambavyo havimhusu. Tabia hiyo yaweza kumuudhi mwenyewe kwani ataweza kuona ya kwamba ana tamaa navyo. Kijumwa anasisitiza kwamba si vyema Helewa kusema ya kwamba angetaka kuwa na vitu kama hivyo vya wenyewe. Kwa maoni yetu tunaona ya kwamba pengine hivyo vitu vikija kupotea Helewa anaweza kushukiwa kwa sababu ya kuonyesha tamaa.Tazama beti hizi:

"Tena baba uwe mtu,
Ukenda nyumba za watu,
Usimshikie zitu,
Ila yeye kukwambia." ub. 7

"Ziku zake za nyumbani,
Usiulize thamani,
Na kunena natamani,
Kama hicho kuzengea." ub. 8

Vilevile, Kijumwa anamshauri kutochezea vitu anavyovipata ama kuvitumia kwa njia yoyote bila ruhusa mfano makasi au wino. Ni kweli kwamba watu wengine wana tabia hii hasi ya kuchezea vitu wanavyovipata bila kujali hisia za mwenye hivyo vitu. Tabia hii ina madhara yake ndiposa

Kijumwa anachukua fursa ya kuikemea mapema. Yawezekana kuviharibu hivyo vitu bila kutarajia na kuleta hasara. Vile tunajua siku hizi kuna magonjwa ya kuambukiza hivyo ni muhimu kujiepusha na tabia ya kutumia vitu vya watu hata kama unahitaji ni muhimu kujizuia na kupata ruhusa kutoka kwa mwenyewe. Tazama beti hizi:

"Makasi kisu meweka,
Wino ukaudirika,
Siinuke na kushika,
Kuteza pasina ndia." ub. 10.

"Ukiona zimekaa,
Zisikutie tama,
Kunyoa kukata nyaa,
Nawe hukuazimia." ub. 11

**4.1.8 Talaka**

Kijumwa katika utenzi wake wa *Siraji* ameshughulikia swala la talaka akimshauri Helewa ya kwamba mke akitaka kuachwa afanye upesi kumwacha ili asije kujuta. Kisha baadaye amtafute mke mwingine. Aidha anamshauri mke atakayeolewa ya kwamba mume atakapotaka kumwacha pia asisitize kuachwa kwa upesi hata kama anampenda ni heri ajizuie. Mawaidha hayo ya Kijumwa tunayapinga kupitia mhimili wa nadharia ya maadili tuliyoitumia kuwa ni 'wajibu wa mwanadamu kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia' Hivyo basi matatizo katika ndoa yanafaa kutatuliwa wala si kutoa talaka kwa upesi vile mtunzi anasema. Matatizo yatokeapo katika ndoa hayafai kuidhuru ndoa kwa kiwango cha kuivunja ila watu wawajibike kwa kujadiliana na kutafuta suluhisho mwafaka. Kwa maoni yetu ni muhimu kuvumiliana na kushauriana katika ndoa ili kukabiliana na changamoto bila kuharibu uhusiano. Tazama beti hizi:

"Na siku ya kukwambia,
Niwata nawe ridhia,
Ni kheri kuitokea,
Ama utaiyutia." ub. 172.

“Wetu binti sikia,
Mwana mume kikwambia,
Akuwata buraia,
Akitinda nena haya.” ub. 174.

**4.1.9 Kutojishughulisha na mambo ya watu.**

Katika ubeti wa 12 na 13 Kijumwa anamshauri Helewa kutojishughulusha na mambo ya watu ambayo hayamhusu. Anamwambia ya kwamba akiwaona watu wakiwa katika shughuli zao hafai kusema pia yeye anataka. Asubiri wakati wake kwani hajui mipango yao. Lakini ikiwa amekaribishwa kujiunga nao ni bora asikatae. Kauli muhimu ya mtunzi katika mawaidha haya ni kuwashauri watu kujishughulisha na mambo muhimu yanayowanufaisha bila kuingilia mambo ya watu na hivyo basi kujiepusha na ugomvi. Tazama beti hizi:

“Uchenda ukawaona,
Watu mbee hunyoana,
Ni makosa ukinena,
Na mimi mai tatia.” ub. 12.

“Na kinyozi mbwa ijara,
Kwa mwenyewe siyo sura,
Huninyoi nami mara,
Kheri kwake kumwendea.’ub.13.

**4.1.10 Utumizi kwa wenzake/ usaidizi**

Katika ubeti wa 15 na 16 Kijumwa anamshauri Helewa ya kwamba rafikiye akihitaji msaada wa kumtuma asikatae bali atii na kumsaidia kwa haraka bila kukawia wala kufanya shughuli zake mwanzo. Hapa mtunzi anasisitiza umuhimu wa watu kusaidiana na kufuata maadili ili kujnga jamii bora yenye amani. Ushauri huu umefasiriwa kwa kutumia mhimili wa nadharia iliyotuongozwa katika utafiti wetu kuwa ‘mwanadamu ana wajibu wa kutekeleza ili kufanya ulimwengu kuwa mahali pa kufurahia.’ Hivyo basi kwa kusaidiana na kutangamana, wanajamii hujiendeleza. Tazama beti hizi:

“Rafiki mwenye ahadi,
Kikutuma msaidi,
Utilie na juhudi,
Shughuli kumfanyia.” Ub. 15.

“Utumwapo sikilia,
Muini sipite ndia,
Ukenda na kutembea,
Nda rudi mara moya.” Ub. 13

Anamshauri Helewa kutokawia anapotumwa wala kudanganya. Anamfahamisha ya kwamba ni muhimu kufanya haki kwa mwenzake na asisononeke. Tunamuunga mtunzi mkono kwa mawaidha haya kwani ni dhahiri ya kwamba mtu anapotumwa anastahili kurejea kwa haraka ili mwenye kumtuma atulie kwa kupata jibu sahihi. Tazama:

“Usinende na pengine,
Na urongo usinene,
Rudi na mwendo asone,
Si haki kulimatia.” ub. 17.

Maadili mengine ambayo Kijumwa ameyashughulikia tofauti na Robert ingawa kwa uchache ni kama yafuatayo: ubishi ubeti 78, kutaniana ubeti 110, Madharau ubeti 41, kutowapiga wanyama ubeti 98 miongoni mwa maadili mengineyo.

### 4.2 Maadili katika utenzi wa *Adili* yanayotofautiana na ya utenzi wa *Siraji*

Katika kijisehemu hiki tumeyachambua maadili ambayo Robert ameyashughulikia katika utenzi wa *Adili* tofauti na yale ambayo Kijumwa ameyashughulikia katika utenzi wa *Siraji.* Maadili hayo ni pamoja na ubinafsi, kutimiza ahadi, chuki miongoni mwa maadili mengineyo.

#### 4.2.1 Ubinafsi

Ubinafsi ni hali ya mtu kujipenda na kujifikiria mwenyewe bila kuwajali wenzake. Kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa, ‘ni binadamu aliye na uwezo wa kuamua mkondo wa mwelekeo wa vitushi,’tumebaini ya kwamba Robert katika utenzi wake wa *Adili* anamshauri Adili ya kwamba asiwe wa kujifikiria mwenyewe tu. Atapata baraka kwa kuwajali wenzake. Hivyo basi, kwa kila akipatacho aweze kugawia wenzake basi asiwe na tamaa kwa kutaka kuchukua kila kitu. Ni kawaida kwamba watu wengi hujitakia

mazuri yote bila kuwajali wenzao na hata kama wanavyo vya kutosha bado wanahitaji zaidi. Hilo si jambo zuri kwa kuwa mtu akiwa na ubinafsi anahatarisha maisha yake mwenyewe na ya wanajamii wenzake. Tazama:

" Kutaka yote wewe,
Wengine wasipewe,
Hakuna heri mwishowe,
Hilo usikusudie." ub. 82

### 4.2.2 Kutimiza ahadi

Ahadi ni agano mtu anatoa kwa mwenzake na ni sharti kutimiza. Ahadi ni deni na mtu kabla ya kutoa ahadi ni bora kufikiria kama ana uwezo wa kutimiza; ndiposa Robert anamshauri mwanaye kwamba kabla ya kutoa ahadi ni sharti awajibike kwa kuipima ikiwa ataitimiza au la na kama hawezi basi ni heri asitoe ahadi hiyo na baadaye kuibadili. Tazama beti hizi:

"Ahadi ni heshima,
Kabla ya kuisema,
Wajibu kuipima,
Ndipo kinywani utoe." ub. 79.

"Ahadi usibadili,
Ila iwe batili,
Sababu ni halali,
Mtu jema achague" ub. 80.

### 4.2.3 Chuki

Chuki ni hali ya mtu kutopenda wenzake au kuwa na kinyongo nao. Chuki mara nyingi hutokana na mzozo baina ya watu au mtu binafsi kuwa na roho mbaya kisha kuwakasirikia wenzake. Robert anamshauri Adili kuwapenda watu wote asitete nao wala kuwa na kinyongo nao. Hivyo basi kwake Robert ni muhimu mtu kuwa na raha siku zote hata kama wenzake wamemkosea asiweke rohoni mwake bali awasamehe. Mawaidha hayo yamefasiriwa na mhimili wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu kuwa 'mwanadamu ana wajibu wa kufanya ulimwengu kuwa

mahali pa kufurahia' Tazama beti hizi:

"Mashavu yasikuvimbe,
Bure na watu ugombe,
Fahamu jino pembe,
Kila mtu mchekee." ub. 84

"Uso wa tabasamu,
Dalili ya ukarimu,
Kiburi uhasimu,
La klwanza lichague." ub. 85.

**4.3 Sababu za kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert**

Sababu za kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert hutokana na maoni yao ya kibinafsi kutegemea na mawaidha yenye kila mmoja alitarajia kumpa mwanaye. Mtunzi Kijumwa ameyashughulikia maadili ya kuhusu talaka ambapo kwao maoni yake ni kwamba ifanywe kwa haraka pale ambapo mke au mume atakapohitaji bila kuchelewa. Yawezekana kwamba mtunzi Kijumwa alishuhudia watu wakijuta baada ya kuwa na subira katika ndoa ambayo yenye mzozo. Ingawa hatukubaliani naye, bila shaka mtunzi huyu ana sababu ya kutoa mawaidha kama hayo kwani katika historia yake Abou (1983) ametufafanulia ya kwamba maisha ya Kijumwa katika ndoa yalikuwa yenye changamoto chungu nzima kwani hata mamake Helewa hawakuwa pamoja anapomwusia ndiposa tunaona ya kwamba pengine alistahamili bila kufaulu ndiposa akaamua kutengana naye.

Sababu nyingine hutokana na mazingira ambayo kila mmoja amekulia. Mtunzi Kijumwa ameyashughulikia maadili ya maakuli pengine kwa sababu katika mazingira yake ya kukulia alishuhudia watu wakiwa na tabia hizo ambazo amezikemea wakati wa kula hasa za kuramba vidole, na kufutia mikono kando ya sinia, kujitengea vipande vikubwa vya nyama, kula kwa tamaa na tabia zingine nyingi amezitaja. Hivyo basi alionelea kwamba ni jambo la muhimu kuwarekebisha wanajamii ili kujiepusha na tabia hasi.

Kwa maoni yetu tunaona ya kwamba watunzi Kijumwa na Robert wametunga tenzi zao

kutokana na tajriba ya kila mmoja wao katika harakati zao maishani. Kazi nyingi za mtunzi Robert zinadhamiria kusawiri umuhimu wa kuishi maisha ya kiadilifu hivyo basi kusisitiza kwake maadili ya kutokuwa na ubinafsi na chuki, kutimiza haki miongoni mwa maadili mengine tofauti na yale Kijumwa ameyashughulikia na hili si jambo geni katika utunzi wake kwani ni desturi yake kutunga kazi zinazosisitiza maadili ya kila aina.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumeweza kuyashughulikia maadili ambayo yanatofautiana katika tenzi za *Siraji* na *Adili*. Aidha tumebaini sababu ya kutofautiana kwa watunzi Kijumwa na Robert. Sura inayofuata ya tano ni hitimisho la utafiti wetu.

## SURA YA TANO
## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa hitimisho la utafiti wetu na kuthibitisha haipothesia zetu na mwishowe kutoa mapendekezo kwa watafiti wengine.

### 5.1. Muhtasari

Katika tasnifu hii tumechunguza maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi mbili za *Siraji* na *Adili*. Tumetumia nadharia ya maadili ambayo inasisitiza kazi ya fasihi kuwa na lengo kuu la kuadilisha jamii. Nadharia hii ya maadili imetuongoza ipasavyo kwa sababu inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kujenga jamii bora yenye maelewano. Tumechunguza maadili kwa vijana wa kiume ambayo yameshughulikiwa na watunzi Kijumwa na Robert katika tenzi zao *Siraji* na *Adili*. Tumelinganisha na kulinganua jinsi watunzi wameyashughulikia maadili hayo na hatimaye tumebaini sababu za kuwiana na kutofautiana kwao.

Katika sura ya kwanza, tumeelezea utangulizi wa utafiti wetu, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na msingi wa nadharia ya maadili na hatimaye mbinu tulizozitumia katika utafiti wetu. Katika sura ya pili, tumejadili dhana ya maadili na dhima yake kisha tumechanganua maadili ambayo yanajitokeza katika utenzi wa *Siraji* na utenzi wa *Adili*. Katika sura ya tatu tumeyashughulikia maadili yanayowiana katika tenzi za *Siraji* na *Adili* na sababu za kuwiana kwao. Kisha baadaye katika sura ya nne tumeyashughulikia maadili ambayo yanatofautiana katika tenzi za *Siraji* na *Adili* na sababu za kutofautiana kwao.

### 5.2 Matokeo

Baada ya utafiti wetu tumebaini ya kuwa watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia maadili kwa vijana wa kiume katika tenzi zao ambapo wamewapa mwongozo wa kuwaelekeza maishani. Utafiti wetu umeonyesha ya kwamba tenzi hizi mbili *Siraji* na *Adili* zina uhusiano wa karibu sana kwani zote zinashughulikia maadili ya vijana wa kiume na maadili hayo

yamefungamanishwa na mafunzo ya dini hasa dini ya Kiislamu.Tumepata ya kwamba Watunzi wa tenzi –*Siraji* na *Adili* wanawiana kwa jinsi wameyashughulikia maadili ya vijana kwa sababu mwelekeo walioutoa umeongozwa na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Isitoshe, tenzi hizi ni wasia wa baba kwa wana wao wa kiume hivyo basi mawaidha yao yanafanana. Tumebaini ya kwamba sababu kubwa ya kuwiana kwa watunzi Kijumwa na Robert ni ya kwamba wote ni waumini wa dini moja ya Kiislamu na ndiposa wakatoa mawaidha ambayo yanathibitika kwenye *Korani* ambacho ni kitabu kitakatifu cha waumini wa dini ya Kiislamu.

Kwa upande mwingine tumebaini kuwa baadhi ya maaadili watunzi Kijumwa na Robert wameyatoa yanatofautiana kwa kiasi fulani. Sababu kubwa ya kutofautiana kwa watunzi hao hutokana na mazingira tofauti waliokulia watunzi na tajriba walizopata kutegemea na mazingira waliokulia.

Katika utafiti huu tulinuia kufanya mambo matatu. Kwanza, tumeonyesha jinsi watunzi wa tenzi *Siraji* na *Adili* wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume katika tenzi zao, pili tumetathimini mwelekeo sawa wa watunzi Kijumwa na Robert na sababu za kuwiana kwao na tatu, tumechunguza jinsi watunzi Kijumwa na Robert wametofautiana katika kushughulikia maadili ya vijana wa kiume na sababu za kutofautiana kwao. Baada ya kufanya utafiti wetu tuligundua kwamba ni ukweli watunzi Kijumwa na Robert wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume. Pia makisio yetu kwamba watunzi hawa wawili wana mwelekeo sawa na uhusiano wa karibu kwa jinsi wameyashughulikia maadili ya vijana wa kiume ni ukweli. Pia tumethibitisha ya kwamba watunzi hawa wa tenzi za *Siraji* na *Adili* wanatofautiana kwa njia moja au nyingine kwa jinsi wameyashughulikia maadili ya wana wao wa kiume.

**5.3 Mapendekezo ya utafiti zaidi**

Tunapendekeza watafiti wengine wa siku zijazo walinganishe na kulinganua maadili ya vijana wa kiume kwa kujikita katika tamthilia, riwaya, au hadithi fupi. Aidha wahakiki wengine wanaweza kushughulikia fani katika kufanikisha maadili katika mojawapo ya tenzi za *Siraji* au *Adili* kwa kutumia nadharia tofauti na yetu ili kuchangia pakubwa ukuaji wa lugha ya fasihi ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Abou, Egl, Mohammad. (1983) *Life and Works of Mohammad Kijumwa*. S.O.A.S, London. Unpublished PHD, Thesis.

Allen, J.W.T (1971) *Tendi.* Nairobi: Heinemann Educational Books.

Arege, T. (2013) *Tunu ya ushairi* Nairobi: Oxford. University Press.

Erikson, H. E (1961) *Youth: Change and Challenge*. New York: America Academy of Art and Science.

Faisy, S.A.S (1984) *Quran Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation.

Gitobu, G. (2014) *Mchango wa Kimaudhui wa Watunzi wa Kike Katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Gudrun, M and & Vierke C. (2010) *Texts from the Dammann Papers and other collections.* Germany: German Research Foundation.

Harries, L. (1962) *Swahili Poetry*, Oxford Clarendom Press.

Hichens, W. (1972) *Al-inkisafi*. S.A. Nasir. Nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1976) *Ushairi wa Shaaban Robert.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kijumwa, M. (1927) *Utendi wa Siraji*. Maktaba ya Lamu Fort. (Haujachapishwa).

Maina, V. (2005) *Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert: Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Manoti, J. (2012) *Dhamira ya Uozo na Athari zake kwa Jamii, katika Riwaya ya Upotevu*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Mazrui, A. na Syambo, B.K. (1992): *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi. East African Educational Publishers.

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya fasihi.* Nairobi. Standard Text Books Graphics and Publishers.

Msokile, M (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O. na Mugenda, G. (1999) Research Methods. Quantitive and Qualitive Approches. Nairobi: Acts Press.

Naliaka R. (2012) *Hali ya Vijana katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara.* Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Nation Media Group (2015) Gazeti la *Taifa Leo*17.10.2015. Nairobi.

……………..……….(2015) Gazeti la *Taifa Leo* 22.12.2015. Nairobi.

………………………(2016) Gazeti La *Taifa Leo* 20.6.2016. Nairobi.

Ngunjiri M. (2012) *Matumizi ya Taswira kama Kigezo cha Kufanikisha Maudhui Katika Utendi Wa Siraji.* Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Njogu K. na Chimerah, R (1999) *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

*nuruyavijana.blogspot.com>2015/12 Fumbuka na Nuru:Utandawazi na Maadili ya Vijana.*

Nyamemba R. (2015) *Uchanganuzi Linganishi wa Swala la Vijana miongoni mwa Watunzi Wanne wa Tunu ya Ushairi*: Tasnifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Obore, E. M. (2012) *Dhuluma Dhidi* ya *Vijana wa Kike katika Riwaya ya Rosa Mistika*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Plato, (1960) *The Republic.* Harmondsworth. Penguin.

Robert, S. (1951) *Kusadikika*. Nairobi: Evans Brothers.

………… (1952) *Utenzi wa Hati.* London: Macmillan.

………….(1952) *Adili na Nduguze.* London: Macmillan.

………….(1959) *Masomo yenye Adili.* Nairobi: Nelson.

………….(1966) *Pambo la Lugha*. Nairobi; Oxford University Press.

…………..(1967) *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini.* Nairobi: Nelson.

………….(1968) *Utubora Mkulima.*London: Nelson.

Senkoro, F. E. (1988) *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: University Press.

Shitemi N.L (2010) *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini.* Nairobi: Oxford University Press.

The Republic of Kenya, (2010) *Kenya Constitution.* Government Printers. Nairobi.

Tolstoy. L N. (1960) *What is Art?* New York. Macmillan Publishing Company.

*www. Tanzaniatoday.co.tz> news> Utandawazi na Maadili ya Vijana*.

Wafula, R. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia tatu kuhusu Wahusika Vijana*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Wafula, R.M. (1992) *Nadharia kama Mwongozo wa Utunzi na Uhakiki*: Makala ya Semina. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wafula, R na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

wa Mberia, K. (1997) *Natala*. Nairobi: Marimba Publications.

…………… (1999) *Maua kwenye Jua la Asubuhi*. Nairobi: Marimba Publications.

…………… (2001) *Kifo Kisimani.* Nairobi: Marimba Publications.

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~muwa Publishers Ltd.

Warner, A na Hichens, W. (1934) *Utendi wa Mwanakupona*. *The Advice of Mwanakupona Upon Wifely Duty*. Medstead: Azania Press.

Watuha, A. (2011) *Maudhui ya Waadhi Katika Utenzi wa Adili:* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Wellek, R.na Warren A. (1973). *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin books Limited.